**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

# HOTUBA YA MHESHIMIWA DOTO MASHAKA BITEKO (MB.), WAZIRI WA MADINI AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA 2019/20




**DODOMA** **MEI, 2019**



Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa akimpongeza Waziri wa Madini Mhe. Doto M. Biteko wakati wa uzinduzi wa Soko la madini ya dhahabu mkoani Geita mwezi Machi, 2019.

# HOTUBA YA MHESHIMIWA DOTO MASHAKA BITEKO (MB.), WAZIRI WA MADINI AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA 2019/20

# VIONGOZI WA WIZARA



**Mheshimiwa Doto Mashaka Biteko (Mb.)**
Waziri wa Madini



**Mheshimiwa Stanslaus Haroon Nyongo (Mb.)**
Naibu Waziri wa Madini



**Prof. Simon Samwel Msanjila**
Katibu Mkuu

# YALIYOMO


**A. UTANGULIZI ......................................................................... 1**

MAJUKUMU NA MALENGO YA WIZARA ................................................... 5

**B. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI YA WIZARA KWA MWAKA 2018/19 ............................................... 7**

I. MIPANGO YA SERIKALI NA VIPAUMBELE VYA WIZARA VILIVYOZINGATIWA ........................................................................ 7

II. MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA MADINI KWA MWAKA 2018/19 ..................................................................................... 8

III. MCHANGO WA SEKTA YA MADINI KWENYE PATO LA TAIFA KWA MWAKA 2018/19 ........................................................................ 9

IV. UENDELEZAJI WA UCHIMBAJI MDOGO WA MADINI ....................... 9

V. UENDELEZAJI WA ENEO LA KIMKATATI KWENYE MIGODI YA MIRERANI ............................................................................... 13

VI. KUHAMASISHA SHUGHULI ZA UONGEZAJI THAMANI MADINI ...... 15

VII. USIMAMIZI WA MATUMIZI YA BARUTI NCHINI .............................. 16

VIII. KUVUTIA WAWEKEZAJI KATIKA SEKTA YA MADINI .......................16

IX. SERA, SHERIA, KANUNI NA TARATIBU ........................................... 18

X. AJIRA NA MAENDELEO YA WATUMISHI ........................................... 21

KAZI ZILIZOTEKELEZWA NA MRADI WA USIMAMIZI ENDELEVU WA RASILIMALI ZA MADINI (SMMRP) ................. 22

I. UKARABATI WA OFISI ZA MADINI ..................................................... 23

II. UJENZI WA VITUO VYA UMAHIRI ..................................................... 23

KAZI ZILIZOTEKELEZWA NA TAASISI ZILIZO CHINI YA WIZARA YA MADINI .............................................................................. 38

I. TUME YA MADINI ........................................................................ 38

II. TAASISI YA JIOLOJIA NA UTAFITI WA MADINI TANZANIA (GST)...47

III. SHIRIKA LA MADINI LA TAIFA (STAMICO) .................................... 52

IV. TAASISI YA UWAZI NA UWAJIBIKAJI KATIKA RASILIMALI MADINI, MAFUTA NA GESI ASILIA (TEITI) ................................................... 57

V. CHUO CHA MADINI ................................................................... 60

VI. KITUO CHA JEMOLOJIA TANZANIA (TGC) ...................................... 63

**C. MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA 2019/20 ............................................... 65**

i. Kuimarisha Ukusanyaji wa Maduhuli ya Serikali Yanayotokana na Rasilimali Madini ........................................ 66
ii. Uanzishwaji na Usimamizi wa Masoko ya Madini ................. 66
iii. Kudhibiti Utoroshaji wa Madini ............................................ 67
iv. Kuendeleza Wachimbaji Wadogo .......................................... 67
v. Kuhamasisha Shughuli za Uongezaji Thamani Madini ...... 68
vi. Kuimarisha Ufuatiliaji na Ukaguzi wa Usalama, Afya, Mazingira na Uzalishaji wa Madini katika Migodi .............. 68
vii. Kuhamasisha Uwekezaji katika Sekta ya Madini ................ 69
viii. Ushiriki wa Watanzania Katika Shughuli za Madini (Local Content) ............................................................................ 69
ix. Kuendeleza Rasilimaliwatu na Kuboresha Mazingira ya Kufanyia Kazi ........................................................................ 70

KAZI ZITAKAZOTEKELEZWA NA TAASISI ZILIZO CHINI YA WIZARA KWA MWAKA 2019/20 ................................................ 71

i. Tume ya Madini ........................................................................ 71
ii. Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini Tanzania (GST)...72
iii. Shirika la Madini la Taifa (STAMICO) ................................... 73
iv. Taasisi ya Uhamasishaji Uwazi na Uwajibikaji katika Rasilimali Madini, Mafuta na Gesi Asilia (TEITI) ................ 73
v. Chuo cha Madini (MRI) ............................................................ 74
vi. Kituo cha Jemolojia Tanzania (TGC) ..................................... 74

**D. SHUKRANI** .............................................................................. **75**

**E. HITIMISHO** ............................................................................. **77**

**VIAMBATISHO** ............................................................................ **79**

# ORODHA YA MAJEDWALI



| Na. | Maelezo ya Jedwali | Namba ya Jedwali |
|---|---|---|
| (a) | Makadirio na Makusanyo Halisi ya Maduhuli kwa Kila Kituo kwa Mwaka 2018/19 pamoja na Makadirio kwa Mwaka 2019/20 | 1. |
| (b) | Takwimu za Mitambo ya Uchenjuaji Dhahabu (Elutions) Nchini | 2. |
| (c) | Kiasi cha Mrabaha na ada ya ukaguzi kilichokusanywa kutoka kwenye madini mbalimbali kuanzia mwezi Julai, 2018 hadi Machi, 2019 | 3. |
| (d) | Kiasi na Thamani ya Madini yaliyouzwa Nje ya Nchi kuanzia Mwaka 2013 - 2018 | 4. |
| (e) | Matukio ya Matetemeko ya ardhi katika maeneo mbalimbali ya Tanzania kuanzia mwezi Julai, 2018 – Machi, 2019 | 5. |

## ORODHA YA PICHA


| Na. | Maelezo ya Picha | Namba ya Picha |
|---|---|---|
| (a) | Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini ilipotembelea Ofisi za Wizara ya Madini, mji wa Serikali Ihumwa. | 1. |
| (b) | Mhe. Dkt John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania akiongea na wachimbaji wadogo katika mkutano uliojumuisha Wachimbaji, Wafanyabiashara na Wadau wa Sekta ya Madini tarehe 22 Januari, 2019 jijini Dar es Salaam | 2. |
| (c) | Soko la Madini ya Dhahabu Mkoa wa Geita | 3. |
| (d) | Muonekano wa Jengo la *One Stop Centre* linalojengwa Mirerani litakapokamilika | 4. |
| (e) | Mhe. Waziri Mkuu akiangalia maonesho ya kwanza ya teknolojia ya uchimbaji na uchenjuaji wa madini ya dhahabu yaliyofanyika mkoani Geita | 5. |
| (f) | Washiriki katika kongamano la *China Tanzania Mining Forum* nchini China | 6. |
| (g) | Maendeleo ya Ujenzi wa Kituo cha Umahiri cha Bariadi | 7. |
| (h) | Maendeleo ya Ujenzi wa Kituo cha Umahiri cha Musoma | 8. |

| Na. | Maelezo ya Picha | Namba ya Picha |
|---|---|---|
| (i) | Maendeleo ya Ujenzi wa Kituo cha Umahiri cha Bukoba | 9. |
| (j) | Muonekano wa Kituo cha Umahiri cha Mpanda kitakapokamilika | 10. |
| (k) | Maendeleo ya Ujenzi wa Kituo cha Umahiri cha Chunya | 11. |
| (l) | Maendeleo ya Ujenzi wa kituo cha Handeni. | 12. |
| (m) | Muonekano wa jengo la Taaluma la MRI Dodoma baada ya kukamilika | 13. |
| (n) | Sehemu ya Mtambo wa Uchenjuaji madini ya dhahabu Lwamgasa - Geita | 14. |
| (o) | Katibu Mkuu Wizara ya Madini Prof. Simon S. Msanjila akimkabidhi Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa STAMICO Kanali Mhandisi Sylvester D. Ghuliku nyaraka na Mtambo wa kuchorongea miamba utakaotumika kufanyia utafiti | 15. |
| (p) | Sehemu ya wataalam kutoka kurugenzi ya Ukaguzi wa Migodi wakifanya ukaguzi katika mgodi wa Buhemba, Mkoani Mara | 16. |
| (q) | Wataalam wa GST wakifanya utafiti wa jiokemia QDS 49 na jiolojia (field checks) iliyopo katika wilaya ya Maswa | 17. |
| (r) | Wataalam wa GST wakifanya uchunguzi katika eneo lililotitia na kutokea shimo kubwa huko Kitopeni Itigi | 18. |

| Na. | Maelezo ya Picha | Namba ya Picha |
|---|---|---|
| (s) | Mtaalam kutoka GST akikusanya takwimu kutoka katika kituo cha kupimia matetemeko ya ardhi mkoani Dodoma | 19. |
| (t) | Naibu Waziri wa Madini Mhe. Stanslaus Nyongo (wa pili kushoto) akikagua mgodi wa Makaa ya Mawe | 20. |
| (u) | Mtambo wa kuchenjua dhahabu wa STAMIGOLD | 21. |
| (v) | Wataalam wa STAMICO wakijaribisha mtambo wa uchorongaji wa kisasa mara baada ya kukabidhiwa jijini Dodoma | 22. |
| (w) | Waziri wa Madini, Mhe. Doto Biteko akihutubia katika warsha iliyoandaliwa na TEITI kwa Kampuni za Madini, Mafuta na Gesi Asilia pamoja na wadau mbalimbali wa tasnia ya uziduaji | 23. |
| (x) | Hatua ya ujenzi iliyofikiwa ya Jengo la taaluma la MRI wakati wa ziara ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini tarehe 13/03/2019 | 24. |
| (y) | Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini ilipotembelea Chuo cha Madini kukagua ujenzi wa Jengo la Taaluma kampasi ya Dodoma tarehe 13/03/2019 | 25. |
| (z) | Vinyago vya miamba na bidhaa za usonara | 26. |

# ORODHA YA VIELELEZO



| Na. | Aina ya Kielelezo | Namba ya Kielelezo |
|---|---|---|
| (a) | Makusanyo ya Maduhuli kutoka aina mbalimbali za madini kuanzia mwezi Julai, 2018 – Machi, 2019 | 1. |
| (b) | Makusanyo ya Maduhuli kutoka aina mbalimbali za madini kuanzia mwezi Julai, 2018 – Machi, 2019 | 2. |
| (c) | Kiasi cha dhahabu kilichozalishwa na kuuzwa nje ya nchi na migodi mikubwa ya dhahabu | 3. |
| (d) | Mwenendo wa Wastani wa Bei ya Dhahabu katika Soko la Dunia kuanzia mwaka 2006 - 2018 | 4. |
| (e) | Mwenendo wa Wastani wa Bei ya madini ya Fedha katika Soko la Dunia kuanzia mwaka 2006 - 2018 | 5. |
| (f) | Ramani inayoonesha vituo nane (8) vya kudumu vya kupimia mitetemo ya ardhi | 6. |

## ORODHA YA VIFUPISHO

| | |
|---|---|
| BLs | Brokers Licences |
| CCTV | Closed Circuit Television |
| Dkt | Daktari |
| DLs | Dealers Licences |
| FYDP | Five Year Development Plan |
| GePG | Government e-Payment Gateway |
| GGM | Geita Gold Mine |
| GST | Geological Survey of Tanzania |
| LAN | Local Area Network |
| LBMA | London Bullion Market Association |
| Mb | Mbunge |
| MLs | Mining Licences |
| MRI | Mineral Resource Institute |
| MROs | Mines Resident Officers |
| MSY | Magonjwa Sugu Yasiyoambukiza |
| NACTE | National Council for Technical Education |
| O.C | Other Charges |
| PCLs | Processing Licences |
| PLs | Prospecting Licences |
| PML | Primary Mining Licences |
| QDS | Quarter Degree Sheet |
| RMOs | Resident Mine Offices |
| SADCAS | Sothern African Development Community in Accreditation Service |
| SML | Special Mining License |
| SMMRP | Sustainable Management of Mineral Resources Project |
| STAMICO | State Mining Corporation |

| | |
|---|---|
| TEHAMA | Teknolojia ya Habari na Mawasiliano |
| TEITI | Tanzania Extractive Industries Transparency Initiative |
| TGC | Tanzania Gemological Centre |
| TIC | Tanzania Investment Centre |
| TML | TanzaniteOne Mining Limited |
| UKIMWI | Upungufu wa Kinga Mwilini |
| VAT | Value Added Tax |
| VVU | Virusi vya Ukimwi |

## HOTUBA YA MHESHIMIWA DOTO MASHAKA BITEKO (MB.), WAZIRI WA MADINI AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA 2019/20

### A. UTANGULIZI

1. ***Mheshimiwa Spika,*** baada ya kupokea taarifa iliyowasilishwa hapa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, ambayo imechambua bajeti ya Wizara ya Madini, naomba sasa Bunge lako Tukufu likubali kupokea, kujadili na kupitisha Taarifa ya utekelezaji wa majukumu kwa Mwaka 2018/19 pamoja na Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Kawaida na ya Maendeleo ya Wizara ya Madini pamoja na Taasisi zake kwa Mwaka 2019/20.

2. ***Mheshimiwa Spika,*** kwanza napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kuijalia nchi yetu amani na utulivu na kutuwezesha kushiriki katika mkutano huu wa 15 wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Vilevile, kwa unyenyekevu namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu kwa mara ya kwanza nikiwa Waziri wa Madini na kwamba ni mara yangu ya kwanza kuwasilisha Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Kawaida na ya Maendeleo ya Wizara.

3. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa namna ya kipekee nitumie fursa hii pia kumshukuru Mheshimiwa **Dkt. John Pombe Joseph Magufuli**, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuniamini na kuniteua kuwa Waziri wa Madini, Wizara ambayo ikisimamiwa

vizuri na kuwa na ufanisi itatoa mchango mkubwa katika ukuaji wa uchumi wa nchi. Aidha, nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa kuendelea kuipa kipaumbele Sekta hii ya Madini kwa miongozo, maelekezo na maagizo mbalimbali anayoyatoa. Napenda kumuahidi Mheshimiwa Rais, Bunge lako Tukufu pamoja na Watanzania wote kwamba mimi pamoja na viongozi wenzangu na wafanyakazi wote wa Wizara ya Madini tutafanya kazi kwa bidii, maarifa na uadilifu mkubwa kwa kadri Mwenyezi Mungu atakavyotujalia ili kuhakikisha kuwa Sekta ya Madini inakuwa na manufaa kwa Watanzania na kuchangia ipasavyo katika Pato la Taifa.

4. ***Mheshimiwa Spika,*** nipende pia kumpongeza kwa dhati Mheshimiwa **Dkt. John Pombe Joseph Magufuli,** Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa uongozi wake mahiri unaoonesha nia ya dhati ya kuhakikisha kuwa rasilimali za nchi zinasimamiwa ipasavyo na kuwanufaisha wananchi wote. Namuomba Mwenyezi Mungu aendelee kumlinda na kumpa nguvu, afya na hekima ili aweze kuendelea kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

5. ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, napenda kumshukuru Mheshimiwa **Samia Suluhu Hassan** Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa maelekezo na miongozo thabiti anayotupatia. Vilevile, napenda kumshukuru Mheshimiwa **Kassim Majaliwa Majaliwa** (Mb.) Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wake makini, ushauri na maelekezo anayoyatoa katika kufanikisha utendaji kazi wa Wizara ya Madini kwa nia ya kuhakikisha rasilimali

madini zinawanufaisha Watanzania na Taifa kwa ujumla.

6. ***Mheshimiwa Spika,*** naomba nitumie nafasi hii vilevile kukupongeza wewe mwenyewe Mheshimiwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Mheshimiwa Naibu Spika kwa namna mnavyolisimamia na kuliendesha Bunge letu Tukufu. Kwa hakika sisi wote ni mashahidi wa namna uongozi wenu ulivyokuwa na ueledi, umakini na wenye kutanguliza mbele maslahi ya Taifa. Kimsingi nipende kusema kuwa tunajivunia kuwa na viongozi wa mfano wa kuigwa kama ninyi. Pia nipende kuwashukuru Wenyeviti wa Bunge kwa namna wanavyokusaidia katika kuliendesha vema Bunge hili ambalo ni mhimili muhimu kwa maendeleo ya watu na Taifa kwa ujumla.

7. ***Mheshimiwa Spika,*** ninawashukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Dustan Luka Kitandula (Mb.), na Makamu Mwenyekiti wake Mheshimiwa Mariamu Ditopile Mzuzuri (Mb.), kwa ushirikiano na ushauri mzuri waliotoa kwa kipindi chote cha 2018/19 ikiwa ni pamoja na kupitia Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Madini kwa Mwaka 2018/19; na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya fedha kwa Mwaka 2019/20. Vilevile, nawapongeza Waheshimiwa wajumbe wa Kamati pamoja na Wabunge wote kwa ujumla wao kwa kazi nzuri wanayofanya ya kutupatia ushauri kwa nyakati tofauti kwani hiyo ndiyo dhana halisi ya kuwawakilisha Wananchi wao.



***Picha Na.1**: Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini ilipotembelea Ofisi za Wizara ya Madini, mji wa Serikali Ihumwa.*

8. ***Mheshimiwa Spika,*** naomba nitumie fursa hii kuwapa pole Waheshimiwa Wabunge waliopata ajali mbalimbali na kuugua katika kipindi hiki. Vilevile, napenda kuungana na Wabunge wenzangu kuwapongeza Mhe. Balozi Dkt. Augustine Philip Mahiga (Mb.), kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Katiba na Sheria, na Mhe. Prof. Palamagamba John Aidan Kabudi (Mb.) kwa kuteuliwa, kuwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki; na Mhe. Angellah Kairuki (Mb.) kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwekezaji).

9. ***Mheshimiwa Spika,*** napenda kwa dhati kabisa kuwashukuru viongozi wenzangu wa Wizara ya Madini, Mheshimiwa Stanslaus Haroon Nyongo (Mb.), Naibu Waziri na Profesa Simon Samwel Msanjila, Katibu Mkuu, viongozi hawa na watendaji wote wa Wizara wananipa ushirikiano mkubwa katika kutekeleza majukumu yangu na kutekeleza majukumu yao kwa kujituma, tija na

ufanisi mkubwa. Kwa pamoja tunakiri kuwa na dhamira moja tu ambayo ni kuhakikisha Sekta ya Madini inaendelea kukua siku hadi siku.

10. ***Mheshimiwa Spika,*** napenda pia kuwapongeza waheshimiwa wabunge waliochaguliwa katika mwaka huu wa fedha 2018/19 kuwawakilisha wananchi. Waheshimiwa wabunge hao ni Mheshimiwa Dkt. Wakili Damas Ndumbaro (Mb.)-Songea Mjini, Mheshimiwa Mhandisi Christopha Kajoro Chiza (Mb.)-Buyungu, Mheshimiwa Maulid Said Abdallah Mtulia (Mb.)-Kinondoni, Mheshimiwa Mwita Mwikabwe Waitara (Mb.)-Ukonga na Mheshimiwa Dkt. Godwin Oloyce Mollel (Mb.)-Siha.

11. ***Mheshimiwa Spika,*** napenda sasa kuchukua fursa hii kuwasilisha Hotuba ya Wizara ya Madini ambayo inatoa Taarifa ya Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa Mwaka 2018/19; Kazi zilizotekelezwa na Taasisi zilizo chini ya Wizara kwa Mwaka 2018/19 pamoja na Mpango, Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka 2019/20.

## Majukumu na Malengo ya Wizara

12. ***Mheshimiwa Spika,*** kutokana na marekebisho yaliyofanyika Mwezi Oktoba, 2017 kupitia Hati Idhini Na.144 ya tarehe 22 Aprili, 2016, Wizara ya Madini ilipewa majukumu yafuatayo:

(a) kubuni, kuandaa na kusimamia Sera, Mikakati na Mipango ya kuendeleza Sekta ya Madini;

(b) kusimamia migodi na kuhamasisha shughuli za uchimbaji pamoja na utafutaji wa madini kwa

kutumia tafiti za kijiofizikia na kijiolojia;

(c) kuratibu na kusimamia uongezaji thamani madini kwenye biashara ya madini;

(d) kukuza ushiriki wa Wazawa kwenye shughuli za utafutaji, uchimbaji na biashara ya madini nchini;

(e) kusimamia na kuratibu shughuli na maendeleo ya wachimbaji wadogo;

(f) kusimamia Taasisi na Mamlaka zilizoko chini ya wizara; na

(g) kuratibu na kusimamia maendeleo na utekelezaji majukumu kwa watumishi wa Wizara.

13. ***Mheshimiwa Spika,*** kulingana na Mpango Mkakati wa Wizara wa Mwaka 2019/20 hadi 2023/24, Malengo Makuu ya Wizara ya Madini ni:

(a) kupunguza maambukizi ya Virusi vya UKIMWI na magonjwa yasiyoambukiza na kutoa huduma kwa waathirika;

(b) kuimarisha na kuendeleza utekelezaji wa Mkakati wa Taifa wa Kupambana na Rushwa;

(c) kuboresha usimamizi na uendelezaji wa rasilimali madini;

(d) kuboresha Sekta ndogo ya uchimbaji madini;

(e) kuimarisha usimamizi wa mazingira katika Sekta ya Madini; na

(ff) kuboresha uwezo wa Wizara katika utoaji wa huduma.

## B. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI YA WIZARA KWA MWAKA 2018/19

### i. Mipango ya Serikali na Vipaumbele vya Wizara vilivyozingatiwa

14. ***Mheshimiwa Spika,*** utekelezaji wa shughuli za Wizara ya Madini katika Mwaka 2018/19 umezingatia Dira ya Taifa ya Maendeleo 2020/25; Mpango wa Pili wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano *(FYDP II)*; Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi kwa kipindi cha Mwaka 2015 – 2020; Sera ya Madini ya Mwaka 2009 na Sheria ya Madini ya Mwaka 2010 kama ilivyorekebishwa Mwaka 2017; na Maagizo mbalimbali ya Viongozi wa Kitaifa. Wizara pia ilizingatia maeneo ya kipaumbele iliyojipangia katika kutekeleza majukumu yake ikiwemo: kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya Serikali yatokanayo na rasilimali madini; kuwaendeleza wachimbaji wadogo na wa kati wa madini; kuhamasisha shughuli za uongezaji thamani madini; kuimarisha ufuatiliaji na ukaguzi wa usalama, afya, mazingira na uzalishaji wa madini katika migodi midogo, ya kati na mikubwa; kuendelea kuhamasisha uwekezaji katika Sekta ya Madini; na kuendelea kuboresha mazingira ya kuwawezesha wananchi kufaidika na rasilimali madini.

## ii. Mapato na Matumizi ya Wizara ya Madini kwa Mwaka 2018/19

15. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Mwaka 2018/19, Wizara ya Madini ilikadiriwa kukusanya jumla ya **shilingi 310,598,007,000** ambapo **shilingi 310,320,004,000** zilipangwa kukusanywa kupitia Tume ya Madini na **shilingi 278,003,000** zilipangwa kukusanywa na Wizara na Chuo cha Madini. Hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2019 Wizara ilifanikiwa kukusanya kiasi **cha shilingi 244,251,470,335.03 sawa na asilimia 78.64** ya lengo la mwaka. Ni matarajio ya Wizara kwamba kufikia Juni 30, 2019 lengo la makusanyo tutalivuka.

16. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka 2018/19, Wizara ya Madini ilitengewa jumla ya **shilingi 58,908,481,992**. Kati ya fedha hizo, **shilingi 39,287,517,992** zilitengwa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida, sawa na **asilimia 66.69** ya bajeti ya Wizara na **shilingi 19,620,964,000** sawa na **asilimia 33.31** zilitengwa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Kati ya fedha za Matumizi ya Kawaida, **shilingi 20,953,262,992** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo na **shilingi 18,334,255,000** ni kwa ajili ya mishahara ya watumishi wa Wizara pamoja na Taasisi zake. Vilevile, kati ya bajeti ya maendeleo iliyoidhinishwa, **shilingi 16,800,000,000** sawa na **asilimia 85.62** ni fedha za ndani na **shilingi 2,820,964,000** sawa na **asilimia 14.38** ni fedha za nje.

17. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2019 Wizara ilipokea jumla ya **shilingi 26,024,655,771** kutoka Wizara ya Fedha na Mipango. Kati ya Fedha hizo, **shilingi**

**25,924,655,771** zilipokelewa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **shilingi 100,000,000** ambazo ni fedha za ndani zilipokelewa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

18. ***Mheshimiwa Spika,*** kati ya fedha za Matumizi ya Kawaida zilizopokelewa, **shilingi 15,409,175,838** zilikuwa kwa ajili ya Matumizi Mengineyo na **shilingi 10,515,479,933** kwa ajili ya matumizi ya Mishahara kwa watumishi wa Wizara na Taasisi zake.

## iii. Mchango wa Sekta ya Madini kwenye Pato la Taifa kwa Mwaka 2018/19

19. ***Mheshimiwa Spika,*** mchango wa Sekta ya Madini katika Pato la Taifa umeendelea kuimarika na kufikia **asilimia 5.07** mwaka 2018. Mchango huo ulitokana na kuongezeka kwa uelewa kwa wadau wa Sekta ya Madini na kuwepo kwa uwazi katika shughuli zao; ukuaji wa sekta; kuimarisha usimamizi wa shughuli za madini kwa kudhibiti utoroshwaji; kuimarisha ukaguzi katika sehemu za uzalishaji na biashara ya madini; kuongezeka kwa viwango vya mrabaha na kuanzishwa kwa ada ya ukaguzi wa madini kupitia Marekebisho ya Sheria ya Madini Sura ya 123 yaliyofanyika mwaka 2017.

## iv. Uendelezaji wa Uchimbaji Mdogo wa Madini

20. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha kuwa changamoto za Sekta ya Madini zinapatiwa ufumbuzi na hivyo kuwafanya wadau kufanya shughuli zao za uchimbaji na biashara ya madini katika mazingira ya kibiashara yanayovutia, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alifanya Mkutano na Wachimbaji, Wafanyabiashara na Wadau wa Sekta ya

Madini tarehe 22 – 23 Januari, 2019 jijini Dar es Salaam.

21. ***Mheshimiwa Spika,*** madhumuni ya mkutano huo ilikuwa ni pamoja na kusikiliza na kupokea changamoto na kero mbalimbali zinazowakabili wachimbaji, wafanyabiashara na wadau wa Sekta ya Madini. Katika mkutano huo Serikali ilipokea kero na hoja mbalimbali zikiwemo: kupunguzwa kwa kodi na tozo zinazotozwa kwa wachimbaji wadogo wa madini; kufutwa kwa maeneo ya leseni za madini zisizoendelezwa; kuwekwa kwa Maafisa Madini kwenye maeneo ya machimbo ya madini; kudhibiti utoroshwaji wa madini; kuimarisha utunzaji wa Mazingira katika maeneo ya uchimbaji madini; ukosefu wa miundombinu na tozo na ada kulipwa kwa fedha za kigeni.

22. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeshazifanyia kazi baadhi ya hoja na kero zilizopokelewa ikiwa ni pamoja na: kuondoa Kodi ya Ongezeko la Thamani *(VAT)* **asilimia 18** na Kodi ya Zuio (*withholding tax)* **asilimia 5** kwa wachimbaji wadogo. Hii inafanya jumla ya kodi zote zilizofutwa kufikia **asilimia 23**. Vilevile, Serikali inaendelea kuifanyia kazi changamoto ya ukosefu wa miundombinu kwa kuanzisha masoko ya madini na kujenga vituo vya mfano na umahiri ambavyo wachimbaji wadogo watapata fursa ya kujifunza teknolojia na mbinu bora na za kisasa za uchimbaji na uchakataji madini na pia watajifunza kuhusu utunzaji wa mazingira. Ni matarajio ya Serikali kuwa hatua hizi zitachangia katika kupunguza utoroshaji wa madini uliokuwa ukifanywa na wachimbaji wadogo wasiokuwa waaminifu na kudhibiti uharibifu wa mazingira.




***Picha Na.2***: *Mhe. Dkt John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania akiongea na wachimbaji wadogo katika mkutano uliojumuisha Wachimbaji, Wafanyabiashara na Wadau wengine wa Sekta ya Madini tarehe 22 Januari, 2019 jijini Dar es Salaam.*

23. ***Mheshimiwa Spika***, katika kuhakikisha kuwa wachimbaji wa madini wanapata masoko rasmi na ya uhakika katika shughuli zao, Serikali kupata mapato stahiki na kudhibiti utoroshaji wa madini nchini, Serikali imeanzisha mfumo wa masoko ya madini katika mikoa yote yenye madini ya metali na vito yaani *metallic Minerals and Gemstones*. Ili kuhakikisha kuwa utekelezaji wa suala hili unaanza mara moja, Wakuu wa Mikoa na Wilaya wameagizwa kutekeleza suala hili ambapo Mkoa wa Geita umetekeleza maelekezo haya kwa kujenga Soko la Madini la Dhahabu. Soko hilo lilizinduliwa na

Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 17 Machi, 2019.

24. ***Mheshimiwa Spika***, nichukue fursa hii kuwapongeza Viongozi wa Mkoa wa Geita kwa kuwa Mkoa wa kwanza kuitikia wito pamoja na mikoa mingine kwa utayari na utekelezaji wao wa haraka ambao unaonesha nia ya dhati ya kuhakikisha Wachimbaji wa madini na Serikali wananufaika na rasilimali madini. Mpaka sasa masoko ya Madini yamefunguliwa katika maeneo mbalimbali ambayo ni Geita, Kahama, Namanga, Singida, Chunya, Ruvuma, Shinyanga, Katavi, Dodoma, Kigoma, Tabora, Mara, Mbeya, Kagera, Iringa, Mwanza, Songwe, Tanga, Manyara na Singida (Sekenke). **Naomba nitoe wito kwa Viongozi wa Mikoa mingine na Wilaya ambazo bado hawajatekeleza maagizo na maelekezo hayo ya Serikali kuharakisha taratibu za uanzishwaji wa masoko katika maeneo yao mapema iwezekanavyo.**




***Picha 3:*** *Soko la Madini ya Dhahabu Mkoa wa Geita*

25. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini Tanzania (GST) iliwapatia mafunzo wachimbaji wadogo **638** kutoka katika vituo sita (6) vilivyofanyiwa utafiti wa kina wa jiosayansi. Vituo hivyo ni Katente-Bukombe, Kyerwa, Buhemba-Butiama, Itumbi-Chunya, D-Reef & Kapanda-Mpanda na Kiomoni-Tanga. Lengo la mafunzo hayo lilikuwa ni kuwaelimisha wachimbaji wadogo kuhusu mbinu za utafutaji, uchimbaji salama, tabia za mbale mbalimbali, uchenjuaji wa madini na utunzaji wa mazingira.

### v. Uendelezaji wa Eneo la Kimkatati kwenye Migodi ya Mirerani

26. ***Mheshimiwa Spika,*** kufuatia kukamilika kwa Ukuta wa Mirerani mwezi Aprili, 2018 udhibiti wa madini ya tanzanite umeimarika na hivyo kuongeza ukusanyaji wa maduhuli yatokanayo na madini hayo. Wachimbaji wadogo Mirerani wameitikia wito wa kulipa kodi na sasa wanalipa kodi kuliko kipindi chochote kwenye historia ya uzalishaji katika eneo hilo. Wachimbaji wadogo Mirerani walikuwa wanachangia kwa **asilimia 6-10** ya mapato yote ya Mirerani; kiasi kikubwa kilikuwa kikichangiwa na TanzaniteOne Mining Limited (TML), kwa mfano katika Mwaka 2017 kiasi cha **shilingi 1,094,228,285.88** kilikusanywa, kati ya fedha hizo **shilingi 930,094,043** zilikusanywa kutoka TML kama mrabaha na ada ya ukaguzi ikiwa sawa na **asilimia 85** ya mapato yatokanayo na uzalishaji wa tanzanite na **shilingi 164,134,242.88** sawa na **asilimia 15** zilikusanywa kutoka kwa wachimbaji wadogo. Kwa mwaka 2018, wachimbaji wadogo pekee wamechangia takribani **shilingi bilioni 1.4** na

uzalishaji umeongezeka kutoka **kilo 147.7** (mwaka 2017) hadi **kilo 781.204** (mwaka 2018) kama inavyooneshwa kwenye **Jedwali Na.1**.

**Jedwali Na. 1: Mchanganuo wa uzalishaji na makusanyo**

| Na. | Mwaka | Kiasi kilichozalishwa (Kg) | Thamani (shilingi) |
|---|---|---|---|
| 1. | 2016 | 164.6 | 71,861,970 |
| 2. | 2017 | 147.7 | 166,094,043 |
| 3. | 2018 | 781.2 | 1,436,427,228 |

27. ***Mheshimiwa Spika***, katika kuhakikisha kuwa mafanikio haya yanakuwa endelevu, Wizara imekwishajenga jengo la wafanyabiashara wa madini yaani *brokers house* na inaendelea na ujenzi wa Kituo cha Pamoja *(One Stop Centre)* ndani ya ukuta unaozunguka machimbo ya tanzanite katika eneo la Mirerani. Wizara vilevile inaendelea kufunga *CCTV cameras* katika eneo hilo. Pia, kwa sasa Wizara inaweka miundombinu ya umeme kuzunguka eneo la ukuta Mirerani. Uwekezaji huo wa Serikali kwa pamoja utagharimu kiasi cha **shilingi 4,284,923,915.98.** Lengo la uwekezaji huo wa Serikali ni: kuhakikisha kuwa shughuli zote zinazohusu biashara ya madini zinafanyika ndani ya ukuta; kuimarisha upatikanaji wa takwimu; na kudhibiti utoroshaji wa madini ya tanzanite.




***Picha 4:*** *Muonekano wa Jengo la Onestop Centre linalojengwa Mirerani litakapokamilika.*

## vi. Kuhamasisha Shughuli za Uongezaji Thamani Madini

28. ***Mheshimiwa Spika***, kazi nyingine iliyotekelezwa na Wizara katika kipindi cha Mwaka 2018/19 ni kukamilisha uandaaji wa Mwongozo wa Uongezaji Thamani Madini na Miamba, 2019 Tangazo la Serikali Na. 60/2019 lililotolewa tarehe **25 Januari, 2019**. Lengo la mwongozo huo ni kuainisha viwango vya uongezaji thamani kwa kila aina ya madini na miamba kabla ya kuruhusiwa kusafirishwa nje ya nchi.

29. ***Mheshimiwa Spika***, vilevile, Wizara imeendelea kushawishi wawekezaji wa ndani na nje ya nchi kuwekeza katika ujenzi wa viwanda vya uongezaji thamani madini hapa nchini *(Smelters and*

*refineries).* Mwezi Februari, 2019 Wizara ilikutana na kufanya majadiliano na kampuni tisa (9) ambazo zimeonesha nia ya kujenga viwanda vya uongezaji thamani madini hapa nchini. Kati ya kampuni hizo tisa, (tatu za Smelters na moja ya Refinery), zimeshawasilisha maombi rasmi ya leseni kupitia Tume ya Madini kama inavyoelekezwa na Sheria ya Madini ya Sura ya 123. Maombi hayo ya leseni yapo katika hatua za mwisho ili hatimaye ziweze kutolewa.

### vii. Usimamizi wa Matumizi ya Baruti Nchini

30. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara iliendelea kusimamia na kudhibiti matumizi ya baruti ikiwa ni pamoja na kuhakikisha watumiaji wa baruti wanaingiza, wanatumia na kutunza baruti kwa usahihi ambapo **vibali 146** vya kuingiza baruti nchini na **leseni 6** za maghala ya kuhifadhia baruti katika maeneo ya Geita na Lugoba vilitolewa. Aidha, jumla ya **tani 32,398** za baruti zilitengenezwa migodini na vipande **3,725,645** vya fataki viliingizwa nchini kwa ajili ya shughuli za ulipuaji kwenye maeneo ya uchimbaji wa madini na ujenzi wa miundombinu. Wizara ilifanya ukaguzi wa maghala **21** ya kuhifadhi baruti katika maeneo ya Lugoba-Pwani, Kilosa- Morogoro na Mirerani-Manyara na kutoa vibali **2** vya kuridhia ujenzi wa maghala mengine mawili katika eneo la Lugoba-Pwani.

### viii. Kuvutia Wawekezaji katika Sekta ya Madini

31. ***Mheshimiwa Spika***, katika kuvutia uwekezaji, Wizara imeendelea kushiriki katika maonesho mbalimbali ya ndani na nje ya nchi. Mwezi Septemba,

2018, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Geita na Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania *(TanTrade)* ilishiriki kuandaa na kufanikisha maonesho ya kwanza ya teknolojia ya uchimbaji na uchenjuaji wa madini ya dhahabu yaliyofanyika mkoani Geita. Maonesho hayo yalishirikisha **kampuni 250** kutoka maeneo mbalimbali nchini, wachimbaji wadogo, wachimbaji wakati, wachimbaji wakubwa, wachenjuaji, wafanyabiashara wa madini pamoja na wadau mbalimbali wa Sekta ya Madini. Maonesho hayo pamoja na mambo mengine yalilenga kuwawezesha wadau kutambua fursa za uwekezaji zilizopo katika Sekta ya Madini.



***Picha 5:*** *Mhe. Waziri Mkuu akiangalia maonesho ya kwanza ya teknolojia ya uchimbaji na uchenjuaji wa madini ya dhahabu yaliyofanyika mkoani Geita*

32. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara pia iliandaa na kushiriki kongamano la kutangaza fursa za uwekezaji katika Sekta ya Madini nchini China lililojulikana kwa jina la *China Tanzania Mining Forum* lililofanyika jijini Beijing tarehe 10 Desemba, 2018. China inasifika kwa kuwa na teknolojia rahisi na nafuu. Hivyo, kongamano hilo lilitumika kuwakutanisha wachimbaji wadogo wa Tanzania na watengenezaji wa mitambo mbalimbali ambayo hutumika kwenye shughuli za uchimbaji na uchenjuaji wa madini. Jumla ya wachimbaji **72** kutoka Tanzania walishiriki katika kongamano hilo wakiwakilisha jumla ya migodi **44**.



***Picha 6:*** *Washiriki katika kongamano la China Tanzania Mining Forum nchini China*

## ix. Sera, Sheria, Kanuni na Taratibu

33. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara inaendelea kufanya mapitio ya Sera ya Madini ya Mwaka 2009 kwa lengo la kuihuisha ili iendane na mazingira ya sasa. Aidha, kwa kushirikiana na Ofisi ya

Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Wizara ilifanikiwa kurekebisha Sheria, Kanuni na Miongozo kama ifuatayo:

*(a)* Sheria ya Madini Sura ya 123 *(Revised Edition 2018);*

(b) Marekebisho ya Sheria ya Uwazi na Uwajikaji katika Rasilimali Madini, Mafuta na Gesi Asilia ya Mwaka, 2015;

*(c)* Kanuni za Jumla za Sheria (Uwazi na Uwajibikaji) katika Sekta ya Madini, 2019, Tangazo la Serikali Na. 141/2019;

(d) Kanuni za Madini (Udhibiti wa Eneo la Mirerani) 2019, Tangazo la Serikali Na.135/2019;

(e) Kanuni za Madini (Biashara ya Almasi), 2019, Tangazo la Serikali Na.137/2019;

(f) Mwongozo wa Uwasilishaji wa Fomu za Ushirikishwaji Bidhaa na Huduma za Watanzania, 2018, Tangazo la Serikali Na.305/2018;

(g) Kanuni za Madini (Kiapo cha Uadilifu) 2018, Tangazo la Serikali Na. 304/2018; na

(h) Mwongozo wa Kuhakiki Uongezaji Thamani Madini au Miamba Nchini kabla ya Madini Kusafirishwa Nje ya Nchi, 2019, Tangazo la

Serikali Na.60/2019.

34. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara pia ilifanya Marekebisho katika Kanuni mbalimbali za Madini chini ya Sheria ya Madini Sura ya 123 kama ifuatavyo: Marekebisho ya Kanuni za Madini (Biashara ya Madini na Makinikia) 2018, Tangazo la Serikali Na. 138/2019; Marekebisho ya Kanuni za Madini (Ushirikishwaji wa Huduma na Bidhaa za Watanzania) 2018, Tangazo la Serikali Na. 139/2019; Marekebisho ya Kanuni za Madini (Uongezaji Thamani Madini) 2018, Tangazo la Serikali Na. 136/2019. Vilevile, Wizara imetafsiri katika lugha ya Kiswahili Kanuni za Utunzaji Mazingira kwa Wachimbaji Wadogo za Mwaka 2010, Tangazo la Serikali Na. 403/2010. Aidha, Wizara imekamilisha Rasimu za Kanuni za Masoko ya Madini, 2019 na Kanuni za Madini (Cheti cha Uasilia), 2019 ambapo rasimu hizi tayari zilishawasilishwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kufanyiwa upekuzi hatimaye kutangazwa katika Gazeti la Serikali.

35. ***Mheshimiwa Spika***, vilevile, mwezi Februari, 2019 Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha na Mipango na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ilishiriki kikamilifu katika mchakato wa Marekebisho ya Sheria mbalimbali uliowezesha Bunge lako tukufu kufanya Marekebisho ya Sheria ya Madini Sura ya 123, Sheria ya Kodi Sura ya 332, Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani Sura ya 148 na Sheria nyinginezo kupitia Sheria ya Marekebisho ya Sheria mbalimbali Na. 6 ya mwaka 2019. Marekebisho hayo yameondoa Kodi ya Ongezeko la Thamani *(VAT* ya asilimia 18*)* na Kodi ya Zuio *(Witholding Tax* ya asimilia 5*)* kwa wachimbaji wadogo wa madini

watakaouza madini yao kupitia masoko ya madini yaliyokwishaanzishwa nchini.

## x. Ajira na Maendeleo ya Watumishi

36. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Mwaka 2018/19, Wizara imepokea na kukamilisha taratibu za ajira mpya kwa watumishi wapya 14 kupitia Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma; na watumishi watano (5) kwa utaratibu wa uhamisho. Aidha, jumla ya watumishi 230 wamehamia Wizara ya Madini kutoka iliyokuwa Wizara ya Nishati na Madini na watumishi 31 wamehamishiwa Tume ya Madini hivyo mpaka mwezi Machi, 2019, Wizara ya Madini ilikuwa na jumla ya watumishi 199.

37. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuwajengea uwezo watumishi wake katika fani mbalimbali ikiwemo Jiolojia, Uhandisi Migodi, Jemolojia, Utunzaji wa Kumbukumbu na Utafutaji wa Madini. Jumla ya watumishi 41 wamepatiwa mafunzo ya muda mfupi na mrefu. Kati ya hao, watumishi 14 wamehudhuria mafunzo ya muda mrefu katika ngazi za: Astashahada (1) Shahada (1); Shahada ya Uzamili (9) na Shahada za Uzamivu (3) na watumishi 27 wamepata mafunzo ya muda mfupi kwenye fani za Jemolojia, Jiolojia, Uhandisi Migodi na Utunzaji wa Kumbukumbu.

38. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kutoa huduma ya lishe na chakula kwa watumishi wanaoishi na virusi vya UKIMWI, ikiwa ni utekelezaji wa Waraka wa Utumishi wa Umma Namba 2 wa

Mwaka 2006 na Mwongozo wa Kudhibiti UKIMWI katika Utumishi wa Umma wa Mwaka 2007.

39. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara pia iliandaa mafunzo kuhusu VVU, UKIMWI na Magonjwa Sugu Yasiyoambukiza (MSY) ambapo wajumbe wa Kamati ya kudhibiti UKIMWI, Maafisa Utumishi, Waelimishaji Rika kutoka katika Idara, Vitengo na Waratibu wa Dawati la VVU, UKIMWI na MSY kutoka Taasisi zilizo chini ya Wizara walishiriki. Katika zoezi hilo, waliojitokeza kupima UKIMWI na MSY walikuwa 97.

40. ***Mheshimiwa Spika,*** moja ya Malengo Makuu ya Wizara ni kuimarisha na kuendeleza Mkakati wa Taifa na Mpango wa Kupambana na Rushwa. Katika kutekeleza lengo hilo, Wizara ilikamilisha uandaaji wa Mkakati wa Kupambana na Rushwa katika kipindi cha 2017/18 - 2021/22. Aidha, watumishi wote wamejaza fomu za kiapo cha kuwa na maadili katika Utumishi wa Umma *(Intergrity Pledge)* kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Umma No. 8 ya 2002, Kanuni za Utumishi wa Umma 2003 pamoja na Kanuni za Maadili ya Utendaji Kazi katika Utumishi wa Umma za mwaka 2005.

**Kazi zilizotekelezwa na Mradi wa Usimamizi Endelevu wa Rasilimali Madini (SMMRP)**

41. ***Mheshimiwa Spika***, lengo kuu la utekelezaji wa mradi wa SMMRP kwa awamu ya pili lilikuwa ni kuboresha shughuli za uchimbaji mdogo nchini ili kuhakikisha wanazalisha kwa tija na hivyo kuchochea kasi ya maendeleo na kupunguza umasikini. Katika kutekeleza lengo hilo, Wizara

kupitia SMMRP imetekeleza shughuli zifuatazo:

### i. Ukarabati wa Ofisi za Madini

42. ***Mheshimiwa Spika***, moja ya kazi zilizotekelezwa na mradi ilikuwa ni ukarabati wa Ofisi za Madini. Ukarabati huo ulifanyika katika Ofisi za Madini Moshi na Nachingwea. Ukarabati katika Ofisi ya Madini Moshi na wa Ofisi ya Madini Nachingwea umekamilika kwa asilimia 100. Kukamilika kwa ukarabati katika Ofisi hizo kumeondoa uhaba wa nafasi za kufanyia kazi kwa watumishi wa Tume waliopo kwenye Ofisi hizo.

### ii. Ujenzi wa Vituo vya Umahiri

43. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Mradi wa SMMRP ilitekeleza ujenzi wa Vituo vya Umahiri saba (7) ambavyo ni Bariadi, Musoma, Bukoba, Mpanda, Chunya, Songea na Handeni. Vituo hivyo vipo katika hatua mbalimbali za ujenzi ambapo kati ya hivyo ujenzi wa vituo vya Bariadi, Musoma, Bukoba, Handeni na Jengo la Taaluma la Chuo cha Madini (Dodoma) umekamilika na ujenzi wa vituo vya Mpanda, Chunya na Songea upo katika hatua za ukamilishwaji.

44. ***Mheshimiwa Spika,*** Lengo la vituo hivyo pamoja na mambo mengine, ni kutoa mafunzo mbalimbali yanayohusu madini kwa wachimbaji wadogo. Aidha, vituo hivyo vitatumika kufanya maonesho ya madini na vifaa vinavyotumika katika shughuli za uchimbaji madini. Aidha, kukamilika kwa ujenzi wa vituo hivyo kutaleta faida zifuatazo: -

- Uwepo wa takwimu za wachimbaji wadogo katika maeneo husika kwa kuwa wachimbaji wadogo watapata fursa ya kujisajili. Taarifa hizi zitaweza kuhuishwa mara kwa mara na pia zitaweza kutumika na Taasisi mbalimbali katika kupanga mipango mbalimbali;
- Wachimbaji wadogo kupata taarifa sahihi za maeneo yaliyotengwa kwa ajili yao;
- Utoaji wa mafunzo na maarifa kwa Wachimbaji wadogo kupitia wadau mbalimbali. Wizara itaweza kuongeza kasi ya utoaji mafunzo kuhusu Sera ya Madini, Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo mbalimbali ya kiutendaji katika shughuli za madini. Vilevile, elimu kuhusu ujasiriamali, utafutaji madini, uchimbaji madini, uchorongaji miamba, mazingira, afya na usalama migodini itatolewa katika vituo hivyo;
- Kutolewa kwa elimu juu ya mfumo wa kutathmini mashapo ya madini yaliyopo ili kufanya uchimbaji wenye tija;
- Kutolewa kwa elimu kuhusu uongezaji thamani madini na upatikanaji wa masoko;
- Usimamizi na uratibu wa shughuli mbalimbali zinazohusu madini; pamoja na
- Utatuzi wa migogoro ya uchimbaji madini inayojitokeza.

Hatua za ujenzi zilizofikiwa katika kila kituo ni kama ifuatavyo:

**Bariadi:**

45. ***Mheshimiwa Spika*,** ujenzi wa kituo cha Bariadi umegharimu jumla ya **shilingi 1,307,836,633.00**. Ujenzi wa jengo hili unajumuisha ujenzi wa jengo kuu (*main Building*), ujenzi wa banda la kuchakatia madini (*Crushing shed*), Kibanda cha Mlinzi (*Auxiliary Building*), kazi za nje (*External works*) ikiwa ni pamoja na ujenzi wa ukuta. Aidha, katika jengo kuu kutakuwa na ukumbi wa mikutano kwa ajili ya mafunzo mbalimbali na maonesho ya shughuli za madini. Vilevile, kutakuwa na maabara ndogo kwa ajili ya kupima sampuli mbalimbali za madini. Kwa sasa ujenzi wa jengo hili upo hatua za mwisho za ukamilishaji.



***Picha Na. 7**: Maendeleo ya Ujenzi wa Kituo cha Umahiri cha Bariadi.*

**Musoma:**

46. ***Mheshimiwa Spika,*** Ujenzi wa kituo cha Musoma umegharimu kiasi cha **shilingi 1,211,861,180.00.** Ujenzi wa jengo hili unajumuisha ujenzi wa jengo kuu (*main Building*), ujenzi wa banda la kuchakatia madini (*Crushing shed*), Kibanda cha Mlinzi (*Auxiliary Building*), kazi za nje (*External works*) ikiwa ni pamoja na ujenzi wa ukuta. Aidha, katika jengo kuu kutakuwa na ukumbi wa mikutano kwa ajili ya mafunzo mbalimbali na maonesho ya shughuli za madini. Vilevile, kutakuwa na maabara ndogo kwa ajili ya kupima sampuli mbalimbali za madini. Kwa sasa ujenzi wa jengo hili umekamilika.



**Picha Na. 8:** *Maendeleo ya Ujenzi wa Kituo cha Umahiri cha Musoma.*

**Bukoba:**

47. ***Mheshimiwa Spika,*** ujenzi wa kituo cha Bukoba umegharimu kiasi cha **shilingi 1,081,453,858.00**. Ujenzi wa jengo hili unajumuisha ujenzi wa jengo kuu (*main Building*), ujenzi wa banda la kuchakatia madini (*Crushing shed*), Kibanda cha Mlinzi (*Auxiliary Building*), kazi za nje (*External works*) ikiwa ni pamoja na ujenzi wa ukuta. Aidha, katika jengo kuu kutakuwa na ukumbi wa mikutano kwa ajili ya mafunzo mbalimbali na maonesho ya shughuli za madini. Vilevile, kutakuwa na maabara ndogo kwa ajili ya kupima sampuli mbalimbali za madini. Kwa sasa ujenzi wa jengo hili umekamilika.



***Picha Na. 9:*** *Maendeleo ya Ujenzi wa Kituo cha Umahiri cha Bukoba.*

**Mpanda:**

48. ***Mheshimiwa Spika***, ujenzi wa kituo cha Mpanda umegharimu kiasi cha **shilingi 1,322,871,134.00** ikiwa ni pamoja na gharama za ununuzi wa samani mbalimbali. Ujenzi wa jengo hili unajumuisha ujenzi wa jengo kuu (*main Building*), ujenzi wa banda la kuchakatia madini (*Crushing shed*), Kibanda cha Mlinzi (*Auxiliary Building*), kazi za nje (*External works*) ikiwa ni pamoja na ujenzi wa ukuta. Aidha, katika jengo kuu kutakuwa na ukumbi wa mikutano kwa ajili ya mafunzo mbalimbali na maonesho ya shughuli za madini. Vilevile, kutakuwa na maabara ndogo kwa ajili ya kupima sampuli mbalimbali za madini. Kwa sasa ujenzi wa jengo hili upo katika hatua za mwisho za ukamilishaji.



***Picha Na.10:*** *Muonekano wa Kituo cha Umahiri cha Mpanda kitakapokamilika*

**Chunya:**

49. ***Mheshimiwa Spika***, ujenzi wa kituo cha Chunya umegharimu kiasi cha **shilingi 1,064,210,237.00** ikiwa ni pamoja na gharama za ununuzi wa samani mbalimbali. Ujenzi wa jengo hili unajumuisha ujenzi wa jengo kuu (*main Building*), ujenzi wa banda la kuchakatia madini (*Crushing shed*), Kibanda cha Mlinzi (*Auxiliary Building*), kazi za nje (*External works*) ikiwa ni pamoja na ujenzi wa ukuta. Aidha, katika jengo kuu kutakuwa na ukumbi wa mikutano kwa ajili ya mafunzo mbalimbali na maonesho ya shughuli za madini. Vilevile, kutakuwa na maabara ndogo kwa ajili ya kupima sampuli mbalimbali za madini. Kwa sasa ujenzi wa jengo hili upo hatua za mwisho za ukamilishaji.



***Picha Na.11:*** *Maendeleo ya Ujenzi wa Kituo cha Umahiri cha Chunya.*

**Songea:**

50. ***Mheshimiwa Spika,*** ujenzi wa kituo cha Umahiri cha Songea umegharimu kiasi cha **shilingi 1,265,448,326.00** ikiwa ni pamoja na gharama za

ununuzi wa samani mbalimbali. Ujenzi wa jengo hili unajumuisha ujenzi wa jengo kuu (*main Building*), ujenzi wa banda la kuchakatia madini (*Crushing shed*), Kibanda cha Mlinzi (*Auxiliary Building*), kazi za nje (*External works*) ikiwa ni pamoja na ujenzi wa ukuta. Aidha, katika jengo kuu kutakuwa na ukumbi wa mikutano kwa ajili ya mafunzo mbalimbali na maonesho ya shughuli za madini. Vilevile, kutakuwa na maabara ndogo kwa ajili ya kupima sampuli mbalimbali za madini.

**Handeni:**

51. ***Mhesimiwa Spika***, ujenzi wa kituo cha Handeni umegharimu kiasi cha **shilingi 1,858,513,526.00** ikiwa ni pamoja na gharama za ununuzi wa samani mbalimbali. Ujenzi wa jengo hili unajumuisha ujenzi wa jengo kuu (*main Building*), ujenzi wa banda la kuchakatia madini (*Crushing shed*), Kibanda cha Mlinzi (*Auxiliary Building*), kazi za nje (*External works*) ikiwa ni pamoja na ujenzi wa ukuta. Aidha, katika jengo kuu kutakuwa na ukumbi wa mikutano kwa ajili ya mafunzo mbalimbali na maonesho ya shughuli za madini. Vilevile, kutakuwa na maabara ndogo kwa ajili ya kupima sampuli mbalimbali za madini. Gharama za ujenzi zimejumuisha na ununuzi wa samani kwa mahitaji ya jengo ikiwemo meza za ofisi, meza za Kompyuta, viti vya kumbi za mikutano vilivyotengenezwa kwa mbao ya Mninga, sofa na makabati ya kuhifadhia nyaraka mbalimbali. Kwa sasa ujenzi wa jengo hili umekamilika.



***Picha Na.12**: Maendeleo ya Ujenzi wa kituo cha Handeni.*

## Chuo cha Madini (MRI) - Dodoma:

52. ***Mheshimiwa Spika***, ujenzi wa jengo la Taaluma la Chuo cha Madini (MRI) - Dodoma umegharimu kiasi cha **shilingi 2,863,161,369.00** ikiwa ni pamoja na gharama za ununuzi wa samani mbalimbali pamoja na vifaa vya ofisi. Aidha, Ujenzi wa jengo hili unajumuisha kazi za nje na ujenzi wa jengo kuu ambalo lina ofisi 35 zenye uwezo wa kuchukua watumishi wawili (2) kila moja, vyumba viwili vya mihadhara vyenye uwezo wa kuchukua watu 100 kwa wakati mmoja, chumba kimoja cha kompyuta chenye uwezo wa kuchukua watu 30, chumba kimoja cha mikutano (*Board Room*) chenye uwezo wa kuchukua watu 30 pamoja na ofisi moja ya pamoja (*Pool Office*) yenye uwezo wa kuchukua watu 10 kwa wakati mmoja. Vilevile, jengo hili litakuwa na ofisi ya mitihani 1 na chumba maalum cha kuhifadhia mitihani *(Strong room)* 1, stoo 1 pamoja na jiko. Gharama za ujenzi zimejumuisha ununuzi wa samani

kwa mahitaji ya jengo ikiwemo meza za ofisi, meza za Kompyuta, viti vya kumbi za mikutano vilivyotengenezwa kwa mbao ya Mninga, sofa na makabati ya kuhifadhia nyaraka mbalimbali. Kwa sasa ujenzi wa jengo hili umekamilika.




***Picha Na.13:*** *Muonekano wa jengo la Taaluma la MRI – Dodoma baada ya kukamilika*

## Vituo vya Mfano vya Lwamgasa, Katente na Itumbi:

53. ***Mheshimiwa Spika***, ujenzi wa mgodi wa mfano na usimikaji wa mitambo ya uchenjuaji wa madini ya dhahabu umefanywa kwa ushirikiano wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano ya Tanzania, Mgodi wa Dhahabu wa GGM pamoja na Serikali ya kijiji cha Lwamgasa mkoani Geita na kimegharimu **shilingi 1,345,040,000**. Aidha, Serikali inaendelea na kazi ya usimikaji wa mitambo ya uchenjuaji wa madini ya dhahabu katika eneo la Katente mkoani Geita ambao utagharimu **shilingi 1,728,953,398.03** na Itumbi

mkoani Mbeya ambao utagharimu **shilingi. 1,715,666,979.28**. Hadi sasa Mradi wa Lwamgasa umekamilika kwa **asilimia 100**, Mradi wa Katente umekamilika kwa **asilimia 50** na Mradi wa Itumbi umekamilika kwa **asilimia 40**.

54. ***Mheshimiwa Spika***, vituo hivi vitakuwa na manufaa makubwa kwa wachimbaji wadogo wanaozunguka maeneo hayo ikiwa ni pamoja na kuwapatia ajira. Vituo hivi vinatarajiwa kutoa mafunzo kwa wachimbaji wadogo wa madini ya dhahabu kuhusu masuala yanayohusu uchimbaji, uchenjuaji, biashara ya madini, afya, usalama migodini, utunzaji wa mazingira, masuala ya kijamii pamoja na masuala mtambuka. Pia, vituo hivi vitatoa huduma ya uchenjuaji kwa wachimbaji wadogo kwa bei nafuu. Nia ni kuwawezesha wachimbaji wadogo waweze kujifunza kwa vitendo ili baadae na wao waweze kuwekeza na kusimika mitambo kama hii ambayo haitumii kemikali za zebaki (mercury) katika uchenjuaji wa madini ya dhahabu. Aidha, Serikali ya Tanzania ikiwa ni Mwanachama wa *Minemata Convetion* ipo kwenye mchakato wa kupunguza ama kuzuia kabisa matumizi ya kemikali ya zebaki katika uchenjuaji wa madini ya dhahabu kwa kuwa, kwa kiasi kikubwa kemikali hizi zimekuwa na athari mbaya sana kwa afya ya binadamu na mazingira kwa ujumla.

55. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa Kituo cha Lwamgasa ambacho pia kimejengwa mgodi wa mfano, wananchi wataweza kujifunza kwa vitendo namna bora ya uchimbaji wa kisasa ikiwa ni pamoja na utengenezaji wa mashimo ya uchimbaji madini

(*mining shaft and drift*) bila kutumia magogo. Teknolojia hii itakuwa na manufaa yafuatayo:-

i. kupunguza kwa kiasi kikubwa ajali migodini kwa kutumia simenti kuimarisha kuta;
ii. kurahisisha utoaji wa mbale mgodini (*haulage system*);
iii. kuongeza maisha ya mgodi (maintain);
iv. kupunguza athari za kimazingira kwa kutokata miti hovyo; na
v. kurahisisha ufungaji wa migodi.

56. ***Mheshimiwa Spika***, ili vituo hivi viwe na tija, ufanisi pamoja na kufikia malengo yaliyokusudiwa, Wizara imeingia makubaliano na Shirika la Madini la Taifa (STAMICO) ya namna bora ya uendeshaji na usimamizi wa vituo hivi ikiwa ni pamoja na kutoza gharama nafuu kwa wachimbaji wadogo watakao kuwa wanaleta mbale ya dhahabu kwa ajili ya uchenjuaji. Kupitia wachimbaji wadogo wa eneo husika, Serikali itaweza kujua kwa uhakika ni kiasi gani cha dhahabu kimepatikana na hivyo kuweza kupata kodi na mrabaha halali kutoka kwa wachimbaji wadogo hao. Aidha, mafunzo yatakayokuwa yanatolewa katika kituo hiki yataboresha namna ya uchimbaji na uchenjuaji wa kitaalam na hivyo kuongeza kipato cha mwananchi mmoja mmoja na Taifa kwa ujumla.



***Picha Na 14:*** *Sehemu ya Mtambo wa Uchenjuaji madini ya dhahabu – Lwamgasa - Geita*

## Mtambo wa Kuchoronga Miamba

57. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara kupitia Mradi wa SMMRP imenunua mtambo wa kuchoronga miamba *(Multipurpose Air Rotary Rig)* uliogharimu **Dola za Marekani 1,128,947**. Mtambo huo umekabidhiwa kwa STAMICO mwezi Desemba, 2018 kwa ajili ya matumizi ya biashara pamoja na kuwasaidia wachimbaji wadogo. Aidha, mtambo huu utatumika katika kufanya utafiti wa kina wa Kijiolojia. Utafiti huu utahusisha uchorongaji wa miamba ambapo taarifa zake zitatumika kujua wingi wa mashapo wa eneo husika, viwango vya mbale, ukubwa na umbali kutoka usawa wa ardhi wa mashapo. Huduma hii itatolewa na Shirika la Madini la Taifa (STAMICO) kwa bei nafuu kwa Wachimbaji Wadogo ambapo taarifa hizo zitawawezesha kujua kiasi cha mashapo kilichopo katika leseni zao na hivyo kuwa na taarifa

maalum *(Bankable document)* itakayowawezesha hata kupata mikopo benki.

58. ***Mheshimiwa Spika,*** Kupitia kazi zitakazofanywa na mtambo huu, Serikali itanufaika kwa mambo yafuatayo:-

-  kupata mapato kupitia kutoa huduma ya Uchorongaji;
-  Kufanya Tafiti za kina kwa manufaa ya Taifa kupitia STAMICO;
-  Kuongeza kipato kwa kiasi kikubwa kwa Wachimbaji Madini watakaopata huduma ya mtambo huu; na
-  Kuongeza pato la Taifa kutokana na Makusanyo yatakayotokana na Wachimbaji waliofanya utafiti wa Kina. *(detail Geoscientific survey).*




**Picha Na 15:** *Katibu Mkuu Wizara ya Madini Prof. Simon S. Msanjila akimkabidhi Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa STAMICO Kanali Mhandisi Sylvester D. Ghuliku nyaraka na Mtambo wa kuchorongea miamba utakaotumika kufanyia utafiti*

**Ununuzi wa Magari**

59. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara kupitia Mradi huo ilinunua magari matatu yaliyogharimu jumla ya **Yen 14,722,940** sawa na fedha za Kitanzania **302,799,486** kwa ajili ya usimamizi wa shughuli za madini.

60. ***Mheshimiwa Spika,*** shughuli nyingine zilizotekelezwa na mradi ni pamoja na: kugharamia uandaaji wa Mpango Mkakati wa Kuendeleza Kituo cha Jemolojia Tanzania ambapo jumla ya **shilingi 185,859,000** zilitumika; ununuzi wa Vifaa vya LAN na TEHAMA kwa ajili ya Ofisi za Madini uligharimu **shilingi 423,860,150.06**; na uandaaji wa Mwongozo wa Mazingira uliogharimu **shilingi 176,000,000**.

**Kazi nyingine zilizotekelezwa na Wizara kwa Mwaka 2018/19**

61. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka 2018/19 Wizara iliandaa na kukamilisha Mpango Mkakati *(Strategic Plan).* Lengo la Mpango huo ni kutoa dira na mwelekeo wa Wizara kwa kipindi cha miaka mitano kuanzia 2019/20 hadi 2023/24. Mpango huo ndio uliotumika katika kuandaa Mpango na Bajeti wa mwaka 2019/20.

62. ***Mheshimiwa Spika,*** rasimu ya Waraka wa Baraza la Mawaziri kuhusu Mapendekezo ya Kutunga Sheria Mpya ya Baruti ya Mwaka 2019 imekamilika. Sheria hiyo pamoja na mambo mengine itasaidia kuwepo kwa mfumo bora wa udhibiti wa matumizi ya baruti ambayo kwa sasa umekosekana.

63. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara pia iliandaa Rasimu mbili (2) za Nyaraka za Baraza la Mawaziri kuhusu maombi ya Leseni mbili (2) za Uchimbaji Mkubwa wa Madini *(Special Mining License - SML).* Lengo la kuandaa na kuwasilisha Nyaraka hizo ni kutokana na Marekebisho ya Sheria ya Madini Sura ya 123 kama ilivyorekebishwa mwaka 2017 ambayo yamefanya Baraza la Mawaziri kuwa Mamlaka inayotoa idhini ya kutolewa kwa leseni za uchimbaji mkubwa wa madini.

## KAZI ZILIZOTEKELEZWA NA TAASISI ZILIZO CHINI YA WIZARA YA MADINI

64. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara ya Madini inasimamia Tume ya Madini; Taasisi ya Jiolojia na Utafiti Madini Tanzania (GST); Shirika la Madini la Taifa (STAMICO); Taasisi ya Uhamasishaji Uwazi na Uwajibikaji katika Rasilimali Madini, Mafuta na Gesi Asilia (TEITI); Chuo cha Madini (MRI); na Kituo cha Jemolojia Tanzania (TGC).

### i. Tume ya Madini

65. ***Mheshimiwa Spika***, lengo kuu la kuundwa kwa Tume ya Madini ni pamoja na kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya Serikali yatokanayo na rasilimali madini; kuimarisha ufuatiliaji wa ukaguzi wa usalama, afya, mazingira, uzalishaji na biashara ya madini katika migodi midogo, ya kati na mikubwa; kudhibiti utoroshaji wa madini; na kuendelea kuboresha mazingira ya kuwawezesha wananchi kufaidika na rasilimali madini.

**Uzalishaji na Ukusanyaji wa Maduhuli**

66. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi kinachoishia mwezi Machi, 2019 jumla ya **kilo 27,550.91** za dhahabu zilizalishwa na kusafirishwa nje ya nchi kutoka katika Migodi Mikubwa na ya Kati. Migodi hiyo ni Geita Gold Mining Ltd, North Mara Gold Mine Ltd, Pangea Gold Mine Ltd (Buzwagi), Bulyanhulu Gold Mine Ltd, Shanta Mining Ltd (New Luika) na STAMIGOLD Biharamulo Mine. Aidha, **kilo 2,214.99** za dhahabu zilizalishwa na wachimbaji wadogo, wachenjuaji na wafanyabiashara wa madini.

67. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi tajwa kiasi cha **karati 309,303.85** za madini ya almasi kilizalishwa katika Mgodi wa almasi wa Mwadui (Williamson Diamond Limited); **karati 3,352.90** katika Mgodi wa El Hilal; na **karati 4,747.45** kutoka kwa wafanyabiashara wa almasi *(Dealers)*. Pia, wachimbaji wadogo wa madini ya tanzanite wamezalisha tanzanite ghafi kiasi cha **kilo 768.75**; tanzanite zilizokatwa na kusanifiwa kiasi cha **karati 87,389.02**; na magonga kiasi cha **kilo 13,146.07**. Aidha, madini mengine ya vito kiasi cha **kilo 534,728.48** kilizalishwa katika maeneo mbalimbali nchini.

68. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa makaa ya mawe jumla ya **tani 603,325.40** zilizalishwa kwenye Mgodi wa Ngaka na Kambas Mining Investment mkoani Ruvuma; **tani 7,370.69** katika Mgodi wa Kabulo – Songwe; na **tani 7,696.96** katika Mgodi wa Edenville – Sumbawanga. Aidha, **tani 13,087,435.48** za madini ya ujenzi na **tani 5,351,227.42** za madini mengine ya viwandani zilizalishwa. Vilevile, **tani**

**9,127.94** za madini ya kinywe zilizalishwa kutoka Mgodi wa GodMwanga Mirerani.

69. ***Mheshimiwa Spika,*** kutokana na uzalishaji huo, jumla ya makusanyo hadi kufikia mwezi Machi, 2019 ilikuwa **shilingi 244,007,016,694.00** sawa na **asilimia 78.63** ya lengo la mwaka la **shilingi 310,320,004,000**. Kati ya makusanyo hayo, **shilingi 223,523,640,306.10** ni mrabaha na ada ya ukaguzi ambayo ni sawa na **asilimia 72** ya lengo la mwaka. Vilevile, kiasi kingine cha makusanyo ya **shilingi 20,483,376,488.94** kilitokana na vyanzo vingine vya mapato ambavyo ni ada ya mwaka, ada za kijiolojia; adhabu mbalimbali; ada ya uchambuzi wa madini; mapato mengineyo; na marejesho ya fedha za Serikali. Napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kuwa hadi kufika Mwezi Juni 30, 2019 tutakuwa tumefikia lengo tulilokuwa tumepangiwa.

**Kudhibiti Utoroshaji wa Madini**

70. ***Mheshimiwa Spika,*** Tume ya Madini kupitia Ofisi zake za Afisa Madini Wakazi *(RMOs)* na Maafisa Migodi Wakazi *(MROs)* ina wajibu wa kusimamia uzalishaji na mauzo ya madini nchi nzima. Utekelezaji wa wajibu huu unasaidia kuimarisha udhibiti wa utoroshaji na biashara haramu ya madini. Katika kuhakikisha kuwa rasilimali madini ambayo tumejaliwa kuwa nazo inakuwa na manufaa kwa Watanzania wote, Tume ya Madini kwa kushirikiana na Vyombo vya Ulinzi na Usalama pia imekuwa ikifanya udhibiti wa utoroshaji wa madini.

71. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia mwezi Februari, 2019 zilikamatwa jumla ya **karati 66.60** za madini ya almasi yenye thamani ya **Dola za Marekani**

**34,782.52** Jijini Dodoma; **gramu 77.20** za madini ya dhahabu zenye thamani ya **shilingi 6,363,995.90** mkoani Tabora; **kilo 75,957.30** za madini ya vito yenye thamani ya **Dola za Marekani 1,795,687.87** Jijini Dar es Salaam; **kilo 5.72** za madini ya dhahabu yenye thamani ya **shilingi 389,789,712.44** mkoani Geita; **gramu 11,445.52** za madini ghafi na **karati 1,351** za vito zenye jumla ya thamani ya **shilingi 206,576,347.05** mkoani Arusha; **tani 3.7** za madini ya aina ya *rhodelite* zenye **thamani ya Dola za Marekani 50,162.46**, mkoani Morogoro; na **kilo 319.594** za madini ya dhahabu yenye thamani ya **Dola za Marekani 11,731,814.20** mkoani Mwanza.

72. ***Mheshimiwa Spika,*** madini yaliyokamatwa katika Mikoa ya Dodoma, Tabora, Mwanza na Dar es Salaam yalitaifishwa na Serikali. Aidha, Madini yaliyokamatwa Mikoa ya Arusha, Morogoro na Geita yapo katika hatua mbalimbali za uchunguzi. Mpaka mwezi Machi, 2019 madini ambayo yalikwishataifishwa yalikuwa na thamani ya jumla ya **shilingi 6,363,995.90** na **Dola za Marekani 13,562,284.59.**

73. ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile katika kudhibiti utoroshaji wa madini nchini, ulinzi umeimarishwa katika maeneo yote ya uzalishaji kwenye migodi mikubwa na ya kati kwa kuwaweka Maafisa Madini Wakazi yaani *Mines Residents Officer* (MROs). Lengo la kuweka Maafisa hao ni kusimamia na kuwasilisha taarifa za uzalishaji wa kila siku pamoja na kudhibiti mianya ya utoroshaji wa madini. Aidha, katika maeneo ya viwanja vya ndege na mipakani wamewekwa wasimamizi kuhakikisha madini yanayopitishwa yana vibali husika na kuzuia

utoroshaji wa madini. **Nitoe wito kwa Watanzania wote kufanya shughuli za madini kwa kuzingatia Sheria za nchi ikiwemo Sheria ya Madini ya Mwaka 2010 kama ilivyorekebishwa Mwaka 2017 pamoja na kanuni zake**. **Kwa kufanya hivyo tutakuwa wazalendo na hivyo kupelekea rasilimali hii tuliyojaliwa na Mwenyezi Mungu kuwa ya manufaa kwa Watanzania wote**.

74. ***Mheshimiwa Spika,*** siku za hivi karibuni kumekuwepo na matukio ya watumishi wasio waaminifu kushirikiana na wachimbaji na wafanyabiashara ya madini wasio waaminifu katika kuibia Serikali mapato kupitia kuwasilisha taarifa zisizosahihi za uzalishaji wa madini. Katika kuhakikisha kuwa tunakomesha tabia hii isiyo ya Kizalendo inayopelekea Serikali kupoteza mapato, Serikali imeendelea kuchukua hatua kali za kinidhamu ikiwemo kuwasimamisha kazi ili kupisha uchunguzi na kuwafikisha mahakamani wale wanaobainika kuwa na makosa. **Niwatake watumishi wote wa Serikali, wachimbaji na wafanyabiashara ya madini kuacha mara moja kushiriki katika vitendo hivyo viovu vinavyorudisha nyuma jitihada za Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania za kuhakikisha rasilimali madini zinawanufaisha Watanzania wote.**

**Utoaji wa Leseni**

75. ***Mheshimiwa Spika,*** Tume ya Madini iliendelea na utoaji wa leseni mbalimbali za madini ambapo hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2019 jumla ya maombi ya **leseni 13,177** yalikidhi vigezo kwa ajili ya kupewa leseni za utafutaji wa madini, uchimbaji mdogo,

uchimbaji wa kati, uchenjuaji wa madini na biashara ya madini. Kati ya maombi hayo, maombi ya leseni za: uchimbaji wa kati wa madini *(MLs)* yalikuwa 74; utafutaji wa madini *(PLs)* 866; uchimbaji mdogo *(PMLs)* 9,728; uchenjuaji wa madini *(PCLs)* 39; leseni kubwa ya biashara madini *(DLs)* 736; na leseni ndogo ya biashara ya madini *(BLs)* 1,734. Kati ya maombi yaliyokidhi vigezo, jumla ya leseni **4,831** zimetolewa katika mchanganuo ufuatao: leseni za uchimbaji wa Kati wa Madini *(MLs)* - 31; leseni za Utafutaji wa Madini *(PLs)* - 76; leseni za Uchimbaji Mdogo *(PMLs)* - 2,244; leseni kubwa za biashara *(DLs)* - 736; leseni ndogo za biashara (BLs) - 1,734; na Leseni za Uchenjuaji wa Madini *(PCLs)* - 10.

76. ***Mheshimiwa Spika,*** Tume ya Madini imeendelea na zoezi la kuhuisha taarifa mbalimbali kuhusu leseni na kubaini leseni zenye mapungufu pamoja na kuandaa Hati za Makosa kwa leseni zilizobainika kuwa na mapungufu. Mapungufu hayo ni pamoja na kuhodhi na kushindwa kuendeleza maeneo ya utafiti waliyopewa; na kushindwa kulipa malipo stahiki ya Serikali ikiwa ni pamoja na ada ya mwaka. Mchanganuo wa Leseni zilizofanyiwa mapitio ni kama ifuatavyo: Leseni za Uchimbaji Mkubwa wa Madini *(SMLs)* – 07 ambapo 2 zimeandikiwa Hati za Makosa; Leseni za uchimbaji wa Kati wa Madini *(MLs)* – 271 ambapo 66 zimeandikiwa Hati za Makosa; Leseni za Utafutaji wa Madini *(PLs)* – 1,509 ambapo 200 zimeandikiwa Hati za Makosa; na Leseni za Uchimbaji Mdogo *(PML)* – 16,356 na kati yake 863 zimeandikiwa Hati za Makosa. Maeneo yote yatakayofutwa yatabaki wazi kwa ajili ya wawekezaji

wenye utayari na uwezo wa kuyaendeleza ikiwemo

wachimbaji wadogo. **Nipende kutoa wito kwa wamiliki wote wa leseni za madini nchini kuzingatia Sheria, Kanuni na taratibu zinazosimamia Sekta ya Madini katika kufanya shughuli zao ili kuondokana na usumbufu usiokuwa wa lazima ikiwa ni pamoja na kufutiwa umiliki wa leseni zao**.

## Ukaguzi wa Migodi

*77.* ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Tume ya Madini ilifanya ukaguzi katika migodi ya Sekenke One Mining Cooperative Society; Nabii Eliya VAT Leaching Plant iliyoko mkoani Singida; migodi ya Pamoja Mining Company Ltd; Nyarugusu Mining Society iliyoko Geita; mgodi wa zamani wa Resolute Tanzania Limited, Eneo la uchimbaji madini la wachimbaji wadogo Mahene mkoani Tabora; Maeneo ya Uchenjuaji wa dhahabu mkoani Tabora, na mgodi wa dhahabu wa chini ya ardhi *(Underground Mine)* wa Bulyanhulu. Kaguzi hizi zilibaini mapungufu katika usimamizi wa masuala ya kiusalama, afya na mazingira pamoja na kuwepo mashimo *(mine pits)* na maeneo hatarishi yenye kemikali *(chemical storage tanks)* yaliyoachwa bila kufukiwa au kuwekewa vizuizi *(barricade).*



***Picha Na. 16:*** *Sehemu ya wataalamu kutoka kurugenzi ya Ukaguzi wa Migodi wakifanya ukaguzi katika mgodi wa Buhemba, Mkoani Mara*

78. ***Mheshimiwa Spika,*** kufuatia mapungufu mbalimbali yaliyobainika, Tume ya Madini ilitoa maelekezo ya kufanyika kwa marekebisho katika migodi hiyo kama ifuatavyo: kufukiwa au kuwekwa vizuizi katika mashimo ya wazi na yasiyotumika; kuzuia wachimbaji kuhifadhi au kuuza baruti bila ya kuwa na vibali; kuhakikisha kuwa wafanyakazi wote katika maeneo ya uzalishaji madini wanatumia Vifaa vya Kinga *(Personal Protection Equipment)*; kuhakikisha kuwa wamiliki wa maeneo ya uchenjuaji madini wanamiliki leseni za uchenjuaji; na kuhakikisha kuwa migodi mikubwa na ya kati inandaa na kutekeleza taratibu endelevu za ufungaji migodi.

## Ushiriki wa Watanzania Katika Shughuli za Madini *(Local Content)*

79. ***Mheshimiwa Spika,*** Tume ya Madini pia iliendelea kusimamia na kuhakikisha kuwa kampuni za

uwekezaji katika Sekta ya Madini zinatumia bidhaa

zinazozalishwa na huduma zinazotolewa na watanzania au kampuni za watanzania kwa mujibu wa Sheria. Katika kufanikisha sharti hili, waombaji wote wa leseni kubwa na za kati za uchimbaji wa madini *(Special Mining License -SML* na *Mining License - ML)* walitakiwa kuwasilisha Mipango kuhusu kutumia bidhaa zinazozalishwa na huduma zinazotolewa na watanzania au kampuni za watanzania *(Local Content Plan)* kwa Tume ya Madini kama kigezo muhimu cha kupata leseni.

80. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka 2018/19 Tume ya Madini ilipitia Mipango 55 ya waombaji wa leseni za utafutaji, uchimbaji na uchenjuaji wa madini ili kuona kama mipango hiyo inakidhi matakwa ya Sheria. Kati ya Mipango hiyo, Mipango ya kampuni 42 iliidhinishwa. Mipango ya Kampuni 13 iliyobainika kuwa na mapungufu ilirejeshwa kwa wahusika kwa ajili ya kufanyiwa maboresho ili kukidhi vigezo vinavyotakiwa.

**Matumizi ya Mfumo wa Serikali wa Kielektroniki katika Ukusanyaji wa Mapato *(GePG-Government e-Payment Gateway)***

81. ***Mheshimiwa Spika,*** Tume ya Madini kama zilivyo Taasisi nyingine za Serikali imeunganishwa kwenye Mfumo wa GePG. Aidha, kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha na Mipango taarifa za makusanyo ya mrabaha zimeboreshwa kwa kuingiza kila aina ya madini yanayoingizwa sokoni katika Mfumo wa *GePG.* Hivyo kwa sasa Tume ina uwezo wa kupata taarifa ya michango ya aina mbalimbali za madini kuhusu makusanyo na tozo za madini kutoka katika Mfumo huo kwa wakati.

### ii. Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini Tanzania (GST)

82. ***Mheshimiwa Spika,*** jukumu kubwa la Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini Tanzania (GST) ni kufanya tafiti za jiosayansi kwa lengo la kuvutia uwekezaji katika Sekta ya Madini. Kupitia tafiti hizi taarifa mbalimbali za jiolojia na uwepo wa madini nchini zinaandaliwa kwa lengo la kuhamasisha uanzishwaji wa migodi mipya. Aidha, GST ina jukumu la kuratibu majanga asili ya jiolojia kama matetemeko ya ardhi, milipuko ya volkano pamoja na maporomoko ya udongo.

#### Ukusanyaji wa Maduhuli

83. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka 2018/19, GST ilikadiriwa kukusanya maduhuli ya **shilingi 371,000,000** kutoka kwenye vyanzo vyake ambavyo ni: tozo za ramani na machapisho ya jiosayansi; tozo za huduma za maabara; na ada za ushauri elekezi. Hadi kufikia mwezi Machi, 2019 jumla ya **shilingi 432,285,137** zilikusanywa. Kiasi hiki ni sawa na **asilimia 117.06** ya lengo lililopangwa kwa mwaka husika.

#### Kufanya Ugani/Tafiti za Jiosayansi na Kuboresha Ramani za Jiolojia na Upatikanaji wa Madini

*84.* ***Mheshimiwa Spika,*** GST ilikamilisha ugani wa jiolojia na jiokemia katika **QDS 202** (mpya) iliyopo Kibaha mkoani Pwani na **QDS 49** *(field checks)* iliyopo katika Wilaya ya Maswa. Taarifa *(Explanatory Notes)*

na ramani zipo katika hatua mbalimbali za ukamilishwaji. Matokeo ya awali ya utafiti huo yanaonesha kuwa kwenye **QDS 202** kuna madini ya chokaa hasa katika maeneo ya Mkulazi yenye ubora wa **asilimia 15** hadi **39**. Aidha, katika **QDS 49** kuna viashiria vya uwepo wa madini ya dhahabu katika eneo la Buhangija; madini ya vito (amethyst) katika maeneo ya Chuli, Sayusayu, Masanwa na Sulu; madini ya *Opal* na chokaa katika eneo la Isagenghe.



***Picha Na.17:*** *Wataalam wa GST wakifanya utafiti wa jiokemia QDS 49 na jiolojia (field checks) iliyopo katika wilaya ya Maswa.*

85. ***Mheshimiwa Spika,*** GST kwa kushirikiana na Taasisi ya Jiolojia ya China *(China Geological Survey – CGS)* ilikamilisha utafiti wa jiokemia kwa skeli kubwa katika Mkoa wa Mbeya na skeli ndogo katika nchi nzima. Utafiti huu ulipelekea kutengenezwa kwa atlasi *(stream sediment atlas)* ya nchi nzima na ya Mkoa wa Mbeya. Atlasi na taarifa hizi zitasaidia kuongeza uelewa juu ya madini yanayopatikana katika eneo lililofanyiwa utafiti. Taarifa hizi pia zinaweza kutumika katika sekta za kilimo, maji, mazingira na masuala ya mipango miji.

86. ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, GST kwa kushirikiana na Taasisi ya Jiosayansi na Rasilimali Madini ya Jamhuri ya Watu wa Korea ya Kusini *(Korea Institute of Geoscience and Mineral Resourcess - KIGAM)* ilikamilisha utafiti wa jiolojia katika maeneo ya QDS 257, 312, 313, 319 na 320 yaliyoko katika wilaya za Momba, Songea na Tunduru. Aidha, kupitia ushirikiano huo, GST ilikamilisha utafiti wa jiofizikia kwa kutumia ndege *(High-resolution airborne geophysical survey)* katika maeneo ya QDS 312 na 313. Uchunguzi wa sampuli katika maabara, uchakataji wa taarifa na uchoraji wa ramani na taarifa zake unatarajiwa kukamilika mwaka ujao wa fedha.

**Tafiti Maalum**

87. ***Mheshimiwa Spika,*** GST ilifanya tafiti maalum ikiwemo utafiti wa jiolojia ili kubaini sababu za kutitia na kutokea kwa mashimo makubwa katika eneo la Kitopeni, Itigi mkoani Singida. Utafiti ulibaini: uwepo wa uwazi uliosababishwa na kuyeyushwa kwa miamba iliyoundwa na madini ya jasi na *calcrete;* na udongo wa eneo hilo ni tifutifu ambao umechangia kubomoka kirahisi baada ya kunyonya maji mengi ya mvua.



***Picha Na.18:*** *Wataalam wa GST wakifanya uchunguzi katika eneo lililotitia na kutokea shimo kubwa huko Kitopeni Itigi*

## Kuboresha Kitabu cha Madini Yapatikanayo Tanzania

88. ***Mheshimiwa Spika,*** GST ilikamilisha ukusanyaji na uchakataji wa takwimu kutoka maeneo mbalimbali katika kila mkoa na kuchora ramani zinazoonesha madini katika mikoa na wilaya zote za Tanzania Bara. Lengo la zoezi hilo lilikuwa ni kuboresha Kanzidata ya Taifa ya Madini na Kitabu cha Madini yanayopatikana Tanzania na matumizi yake.

## Huduma za Maabara

89. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi kinachoishia tarehe 31 Machi, 2019, GST ilifanya uchunguzi wa madini katika **sampuli 10,740** ikilinganishwa na lengo la **sampuli 7,500** ililojipangia. Uchunguzi huu ulilenga kubaini uwepo, ubora, na kiasi cha madini katika sampuli hizo. Ongezeko la sampuli limetokana na marekebisho ya Sheria ambayo inaweka sharti la sampuli zote za

madini kufanyiwa uchunguzi kabla ya kusafirishwa nje ya nchi. Aidha, katika kuhakikisha kuwa GST inaendelea kutoa huduma zake za maabara zinazokidhi viwango vya kimataifa, maboresho ya mifumo ya uendeshaji wa huduma zake yalifanyika na kukaguliwa na Taasisi ya SADCAS. Taaasisi hii ni mojawapo ya Taasisi zinazosimamia ubora wa huduma zinazotolewa na Maabara duniani kote.

90. ***Mheshimiwa Spika,*** kupitia ukaguzi huo, Maabara ya GST iliweza kukidhi vigezo vya kimataifa katika uchunguzi wa Madini ya dhahabu na menejimenti ya maabara kwa ujumla na kupendekezwa kupewa ITHIBATI (*Recommended for accreditation).* Ni matumaini yangu kuwa maabara ya GST itaendelea kuwa ni maabara bora inayotoa huduma zake kwa kuzingatia viwango vya kimataifa na hivyo kuwa mojawapo ya maabara bora Afrika.

## Kuratibu Majanga ya Asili ya Jiolojia

91. ***Mheshimiwa Spika,*** jukumu lingine la GST ni kuratibu majanga asili ya jiolojia na kutoa ushauri wa namna bora ya kupunguza madhara yanayoweza kusababishwa na majanga hayo. Katika kutekeleza jukumu hili, GST ilikusanya na kuchakata takwimu za matetemeko ya ardhi kutoka **vituo 9** vya kudumu vilivyopo Kondoa, Babati, Arusha, Geita, Kibaya, Manyoni, Mbeya, Mtwara na Dodoma. Matukio mengi yalikuwa madogo hivyo hayakuwa na madhara kwa umma isipokuwa tetemeko la ardhi la ukubwa wa kipimo cha ritcher 5.1 lililoleta athari zaidi katika mkoa wa Mbeya. Madhara ya tetemeko hilo yalikuwa ni pamoja na kifo cha mtu mmoja katika mkoa wa Songwe na uharibifu wa majengo mkoani Mbeya.



**Picha Na.19:** *Mtaalam kutoka GST akikusanya takwimu kutoka katika kituo cha kupimia matetemeko ya ardhi mkoani Dodoma*

92. ***Mheshimiwa Spika,*** GST pia ilichakata takwimu za matukio ya matetemeko ya ardhi ambayo yamewahi kutokea katika kipindi cha mwaka 1966 hadi 2017 ili kubaini vitovu na mipasuko ya miamba katika eneo linalojengwa Mji wa Serikali, Dodoma. Taarifa iliandaliwa na kuwasilishwa kwa Kamati ya Ujenzi ya mji huo. Matokeo yalionesha kuwa: hakuna kitovu cha matetemeko ya ardhi katika eneo la mradi. Aidha, takwimu za utafiti wa jiolojia katika skeli kubwa *(Regional scale)* zimebaini eneo la mradi wa ujenzi wa mji wa Serikali lipo kwenye miamba ya *tonalite* na *tonalitic orthogneiss* ambayo ni sehemu ya tabaka la miamba imara.

## iii. Shirika la Madini la Taifa (STAMICO)

93. ***Mheshimiwa Spika,*** STAMICO imeendelea kutekeleza majukumu yake kama yalivyoainishwa katika Hati ya Kurekebisha Uanzishwaji wa STAMICO

*(The Public Corporation State Mining Corporation Establishment Amendments Order, 2015).* Majukumu hayo ni pamoja na: kuwekeza kwenye shughuli za uchimbaji na utafutaji madini; kuwekeza katika uchenjuaji, uongezaji thamani na uuzaji madini; na kutoa huduma na ushauri wa kitaalam na kiufundi katika Sekta ya Madini ikiwemo wachimbaji wadogo kwenye nyanja za jiolojia, uhandisi, mazingira na uchorongaji miamba.

**Mradi wa Makaa ya Mawe wa Kiwira – Kabulo**

94. ***Mheshimiwa Spika,*** Shirika linaendelea na uchimbaji na uuzaji wa makaa ya mawe katika mradi wa Kabulo uliopo mkoani Songwe. Kwa sasa uzalishaji unafanyika katika eneo la Kabulo na ulianza mwezi Novemba, 2018. Hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2019, STAMICO imefanikiwa kuchimba jumla ya **tani 22,119** za makaa ya mawe ambapo **tani 7,664.8** zimeuzwa katika kipindi hiki kwa watumiaji mbalimbali wa ndani na nje ya nchi. Aidha, Mgodi umeweza kulipa mrabaha wa **shilingi 12,812,022.78**, ada ya ukaguzi ya **shilingi 4,270,674.26** pamoja na tozo mbalimbali zinazofikia **shilingi 19,745,636.15**.



***Picha Na.20:*** *Naibu Waziri wa Madini Mhe. Stanslaus Nyongo (wa pili kushoto) akikagua mgodi wa Makaa ya Mawe*

## Mgodi wa Dhahabu STAMIGOLD

95. ***Mheshimiwa Spika,*** STAMIGOLD ni kampuni tanzu ya Shirika la Madini la Taifa inayomilikiwa na STAMICO na Msajili wa Hazina. Hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2019 mgodi wa STAMIGOLD umezalisha jumla ya **wakia 9,879.8** za madini ya dhahabu na **wakia 1,346.92** za madini ya fedha yenye thamani ya jumla ya **Dola za Marekani 12,353,394.44** sawa na **shilingi bilioni 28.267**. Mauzo hayo yameuwezesha mgodi kulipa mrabaha wa **shilingi bilioni 1.696** na

ada ya ukaguzi ya **shilingi milioni 282.67** kwa Serikali.



**Picha Na 21:** *Mtambo wa kuchenjua dhahabu wa STAMIGOLD*

96. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka 2018/19, Shirika lilipata mafanikio yafuatayo: kukamilisha ukarabati wa kinu cha kusagia makaa ya mawe kwa lengo la kuongeza thamani ya makaa yanayochimbwa katika Mgodi wa Kabulo ili kukidhi mahitaji ya soko; kupata zabuni ya uchorongaji miamba kwa kutumia njia ya *Reverse Circulation (RC)* kwenye Mgodi wa dhahabu wa Buckreef kiasi cha **mita 1,719**; na kukamilisha ukarabati wa nyumba nne (4) za makazi katika Mradi wa Kiwira pamoja na matengenezo ya magari mawili (2) ya mizigo yatakayotumika kubeba makaa ya mawe kutoka mgodini hadi eneo la kuuzia. Shirika pia lilipokea na kuufanyia majaribio mtambo

wa uchorongaji ulionunuliwa na mradi wa SMMRP kwa ajili ya uendelezaji wa uchimbaji mdogo nchini.



***Picha Na.22:*** *Wataalam wa STAMICO wakijaribisha mtambo wa uchorongaji wa kisasa mara baada ya kukabidhiwa jijini Dodoma*

97. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Mwaka 2018/19 shirika limefanikiwa kutoa gawio la **shilingi bilioni 1** ikiwa ni miaka mingi tangu shirika lianze kujiendesha kibiashara. Gawio hilo limetokana na mapato ya vyanzo vyake vya ndani pamoja na mapato ya kampuni tanzu ya Shirika ya kuchimba dhahabu ya Biharamulo (STAMIGOLD) ambapo kwa mwaka 2018 Shirika linaweza kutengeneza faida na hivyo kutoa gawio kwa serikali.

98. ***Mheshimiwa Spika,*** nipende kuwahakikishia watanzania kuwa Shirika litaendelea kutoa gawio kwa Serikali kwa kuongeza wigo wa vyanzo vyake vya mapato. Aidha, ni matumaini ya Wizara kuwa kufuatia hatua zinazoendelea kuchukuliwa, STAMICO itaendelea kuimarika na kuwa Shirika la Umma litakaloendesha miradi yake kwa faida kwa niaba ya Serikali.

### iv. Taasisi ya Uwazi na Uwajibikaji katika Rasilimali Madini, Mafuta na Gesi Asilia (TEITI)

99. ***Mheshimiwa Spika,*** kazi za TEITI ni kuhamasisha uwazi na uwajibikaji hususan katika uvunaji wa rasilimali madini, mafuta na gesi asilia ili kuongeza manufaa yanayotokana na shughuli za utafutaji na uchimbaji wa rasilimali hizo nchini. Aidha, TEITI ina jukumu la kuhakikisha kampuni zinazofanya shughuli za utafutaji na uchimbaji wa madini, mafuta na gesi asilia zinaweka wazi taarifa za shughuli zao kulingana na Sheria iliyoianzisha TEITI (TEITA) ya mwaka 2015. Maeneo ya uwazi yanayolengwa ili nchi iweze kunufaika ni:- utoaji wa leseni na mikataba ya uchimbaji wa madini, mafuta na gesi asilia; ukusanyaji wa mapato; na mgawanyo wa mapato na matumizi yatokanayo na rasilimali hizo.

100. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha kuwa uwazi na uwajibikaji katika matumizi ya fedha za Serikali zinazotokana na shughuli za madini, mafuta na gesi asilia, TEITI imekamilisha muhtasari wa takwimu zilizowekwa katika vielelezo kwa lugha ya kiswahili na kiingereza za ripoti ya TEITI ya Mwaka 2015/16 kwa ajili ya kufanya wepesi wa kufikisha matokeo ya ripoti hizo kwa wadau. Lengo ni kuleta uwazi na uwajibikaji katika matumizi ya fedha za Serikali zinazotokana na shughuli za Madini, Mafuta na Gesi Asilia.

101. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuhakikisha kuwa taarifa za TEITI zinawafikia wadau kwa njia rahisi, TEITI kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, Tawala za

Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) walikamilisha kazi ya kutengeneza Mfumo wa Kieletroniki kwa ajili ya kuweka Takwimu za TEITI katika vielelezo *(Dashboard). Dashboard* hii ni chanzo cha taarifa zinazohusiana na Sekta ya Uziduaji Tanzania; chombo *(visualization tool)* kinachowezesha watumiaji kuelewa na kuhoji kuhusu takwimu zilizopo katika ripoti za TEITI kwa urahisi; itaonesha mapungufu katika takwimu zilizopo na kutoa nafasi kwa wananchi kuishauri TEITI juu ya kuboresha na kutoa takwimu bora. *Dashboard* hii inapatikana kupitia *http://dashboard.teiti.go.tz/.*

102. ***Mheshimiwa Spika,*** tarehe 11 Aprili, 2019 TEITI ilifanya warsha ya siku moja kwa lengo la kuelimisha Kampuni za Madini, Mafuta na Gesi Asilia kuhusu wajibu na majukumu ya TEITI. Aidha, elimu ilitolewa juu ya wajibu wa Kampuni za Madini, Mafuta na Gesi Asilia katika kutekeleza Sheria ya Uwazi na Uwajibikaji ya Mwaka, 2015 pamoja na Kanuni zake za Mwaka 2019. Kwa mujibu wa Sheri hiyo makampuni yana wajibu wa: kuweka wazi malipo yote ya Kampuni kwa Serikali; kuweka wazi mikataba ambayo kampuni ziliingia na Serikali, na kuweka wazi wamiliki wa hisa katika Kampuni za Madini, Mafuta na Gesi Asilia.

103. ***Mheshimiwa Spika,*** warsha hii ilihudhuriwa na washiriki zaidi ya 130. Washiriki walitoka: Kampuni za Madini, Mafuta na Gesi Asilia; Wadau wa Maendeleo; Asasi za Kiraia; Wajumbe wa Kamati ya TEITI; na Waandishi wa Habari. Mada mbalimbali zilitolewa ikiwemo: utekelezaji wa shughuli za EITI nchini; wajibu wa Kampuni za Madini, Mafuta na Gesi

Asilia katika utekelezaji wa shughuli za EITI; wajibu

wa shughuli za Asasi za Kiraia pamoja na Serikali katika kutekeleza shughuli za EITI nchini.

104. ***Mheshimiwa Spika,*** TEITI kwa kushirikiana na *Natural Resources Governance Institute* (NRGI) waliendesha mafunzo kuhusu uwekaji wazi majina ya wamiliki wa hisa katika kampuni za Madini, Mafuta na Gesi Asilia *(Disclosure of Beneficial Ownership).* Lengo la mafunzo hayo lilikuwa ni kuelimisha washiriki kuhusu umuhimu wa kuweka wazi majina ya wamiliki wa hisa katika Kampuni za Madini, Mafuta na Gesi Asilia. Kufuatia mafunzo hayo, TEITI imeendelea kuhamasisha wadau mbalimbali kuhusu umuhimu wa kuweka wazi majina ya wamiliki wa hisa katika kampuni zao ambayo yatawekwa kwenye rejista na tovuti ya TEITI.




**Picha Na.23:** *Waziri wa Madini, Mhe. Doto M. Biteko akihutubia katika warsha iliyoandaliwa na TEITI kwa Kampuni za Madini, Mafuta na Gesi Asilia pamoja na wadau mbalimbali wa tasnia ya uziduaji.*

## v. Chuo cha Madini

105. ***Mheshimiwa Spika,*** lengo kubwa la kuanzishwa kwa Chuo cha Madini ni kutoa mafunzo ya Ufundi Sanifu katika Sekta ya Madini ili kuzalisha wataalam wa kada ya kati *(technicians).* Chuo kina kampasi mbili ambazo ni kampasi ya Dodoma na kampasi ya Nzega. Mafunzo yatolewayo na Chuo cha Madini yamegawanyika katika aina kuu tatu: mafunzo ya muda mrefu, mafunzo ya muda mfupi

pamoja na mafunzo maalumu (*Tailor-made courses*) yanayoandaliwa kulingana na mahitaji ya wadau.

106. ***Mheshimiwa Spika,*** fani zinazofundishwa na Chuo cha Madini ni pamoja na: Jiolojia na Utafiti wa Madini; Sayansi za Mafuta na Gesi; Uhandisi Uchimbaji Madini; Uhandisi Uchenjuaji Madini; Uhandisi wa Mazingira na Usimamizi wa Migodi; na Upimaji Ardhi na Migodi. Mafunzo haya yanatolewa kwa mfumo wa umahiri ambapo msisitizo mkubwa ni kutekeleza mafunzo kwa vitendo.

**Udahili wa Wanafunzi**

107. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa masomo wa 2018/19, Chuo kilidahili jumla ya wanafunzi **600** kwa kampasi zote mbili za Dodoma na Nzega sawa na ongezeko la **asilimia 11.9** ikilinganishwa na wanafunzi **536** waliodahiliwa mwaka 2017/18. Kati ya hao, wanafunzi **503** walidahiliwa kampasi ya Dodoma na **97** kampasi ya Nzega. Wanafunzi **91** walidahiliwa katika fani za Jiolojia na Utafutaji Madini*;* **99** katika Uhandisi Uchimbaji Madini*;* **144** katika Uhandisi Uchenjuaji Madini; **63** katika Uhandisi wa Mazingira na Usimamizi wa Migodi; **99** katika Sayansi za Mafuta na Gesi; na **104** katika Upimaji wa Ardhi na Migodi

**Ukusanyaji wa Maduhuli**

108. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka 2018/19, Chuo cha Madini kilikadiriwa kukusanya maduhuli ya jumla ya **shilingi 268,000,000**. Hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2019, Chuo kilikuwa kimekusanya jumla ya **shilingi 242,603,540** sawa na **asilimia**

**90.52** ya lengo. Makusanyo haya yalitokana na ada ya mafunzo, usajili na malazi.

**Kuboresha miundombinu ya Chuo cha Madini katika Kampasi ya Dodoma na Nzega**

109. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai, 2018 hadi tarehe 31 Machi, 2019, Chuo kimeendelea kuboresha miundombinu yake ikiwemo ukarabati wa majengo na mazingira ya kufundishia na kujifunzia. Ukarabati umefanyika katika majengo ya madarasa, mabweni, nyumba za watumishi, pamoja na jengo la utawala ikihusisha pia kufanya ukarabati katika mifumo ya umeme, maji safi na maji taka katika Kampasi ya Nzega.



**Picha Na 24:** *Hatua ya ujenzi iliyofikiwa ya Jengo la taaluma la MRI wakati wa ziara ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini tarehe 13/03/2019*



**Picha Na. 25:** *Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini ilipotembelea Chuo cha Madini kukagua ujenzi wa Jengo la Taaluma kampasi ya Dodoma tarehe 13/03/2019*

**Kusajili Kampasi ya Nzega kwenye Baraza la Taifa la Mafunzo ya Ufundi (NACTE)**

110. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka 2018/19, Chuo kilifanikiwa kupata usajili kamili wa Kampasi ya Nzega kwenye Baraza la Taifa la Mafunzo ya

Ufundi (NACTE) na kupewa namba ya usajili **REG/SAT/041**. Usajili huu umekifanya Chuo cha Madini kampasi ya Nzega kutambuliwa na NACTE kama kituo cha kutolea mafunzo ya muda mrefu na mfupi katika fani za Madini, Mafuta na Gesi.

### vi. Kituo cha Jemolojia Tanzania (TGC)

111. ***Mheshimiwa Spika,*** majukumu ya Kituo cha Jemolojia Tanzania (TGC) ni pamoja na: kutoa mafunzo ya muda mrefu (stashahada) katika fani za usanifu wa madini ya vito na teknolojia ya kutengeneza vito; utambuzi, ukataji na kutengeneza vito; na kutoa huduma za kusanifu madini ya vito, miamba, utengenezaji wa bidhaa za mapambo na urembo (usonara) pamoja na kutoa mafunzo ya muda mfupi katika fani ya ukataji na ung'arishaji wa madini ya vito.



**Picha Na. 26:** Vinyago vya miamba na bidhaa za usonara

## Udahili wa Wanafunzi

*112.* ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka 2018/19 Kituo kilidahili jumla ya wanafunzi 26 katika fani za usanifu wa madini ya vito, utambuzi wa madini ya vito na usonara. Aidha, katika kipindi husika jumla ya wanafunzi 23 walihitimu mafunzo ya ukataji na ung'arishaji madini ya vito kwa ngazi ya cheti. Kituo pia kilizalisha bidhaa zitokanazo na miamba, madini ya vito na usonara kama ifuatavyo vinyago 64, hereni 72, vikuku 40, miti ya mawe 15, mikufu 24, vidani 50, *beads* kilo 21 na vito vilivyokatwa *amethyst 35.35 carats, citrine 25.3 carats, white quartz 102.45 carats, garnet 78.6 carats, moldavite 1,780.3 carats, iolite 64.45 carats* na *moonstone 341.5 carats*.

## C. MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA 2019/20

113. ***Mheshimiwa Spika,*** uandaaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara kwa Mwaka 2019/20 umezingatia Dira ya Taifa ya Maendeleo 2020/25; Mpango wa Pili wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano (FYDP II); Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi kwa kipindi cha Mwaka 2015 – 2020; Sera ya Madini ya Mwaka 2009; Sheria ya Madini Sura ya 123 na Marekebisho yake ya Mwaka 2019; Maagizo mbalimbali ya Viongozi wa Kitaifa; Mwongozo wa Kutayarisha Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2019/20.

114. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka 2019/20, Wizara imejiwekea maeneo yafuatayo ya kipaumbele:- kuimarisha ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali yatokanayo na rasilimali madini; uanzishwaji na usimamizi wa Masoko ya Madini; kudhibiti utoroshwaji wa madini; kuendeleza uchimbaji mdogo na wa kati wa madini; kuhamasisha shughuli za uongezaji thamani madini; kuimarisha ufuatiliaji na ukaguzi wa usalama, mazingira na uzalishaji wa madini katika migodi midogo, ya kati na mikubwa; kuhamasisha uwekezaji katika Sekta ya Madini; kuboresha mazingira ya kuwawezesha Wananchi kunufaika na rasilimali madini; na kuendeleza rasilimaliwatu na kuboresha mazingira ya kufanyia kazi.

### i. Kuimarisha Ukusanyaji wa Maduhuli ya Serikali Yanayotokana na Rasilimali Madini

115. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka 2019/20, Wizara inapanga kukusanya **shilingi 470,897,011,000** ikilinganishwa na **shilingi 310,598,007,000** kwa Mwaka 2018/19 sawa na ongezeko la **asilimia 51.62**. Mikakati itakayotumika kufikia lengo hilo ni pamoja na: kusimamia masoko ya madini; kuimarisha ukaguzi wa migodi mikubwa, ya kati na midogo ili kupata taarifa sahihi za uwekezaji, uzalishaji, mauzo, tozo na kodi mbalimbali; kudhibiti utoroshwaji wa madini katika maeneo yote nchini; kuimarisha ukaguzi wa madini ya ujenzi na viwandani; kufuatilia taarifa za ununuzi na uuzaji *(returns)* kwa wafanyabiashara wa madini *(Dealers & Brokers)*; kufuatilia wadaiwa wa tozo mbalimbali za madini kwa mujibu wa Sheria kwa wakati; kudhibiti uchimbaji na uchenjuaji haramu wa madini; na kuboresha na kuimarisha Mfumo wa kutolea leseni za madini na kutunza taarifa zake.

### ii. Uanzishwaji na Usimamizi wa Masoko ya Madini

116. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuhakikisha kuwa wachimbaji wadogo wananufaika na shughuli za uchimbaji madini, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi za Wakuu wa Mikoa imeanzisha na inaendelea kuanzisha Masoko na kuendesha Minada ya Madini katika maeneo mbalimbali nchini. Nia ya jitihada hizi ni kutatua tatizo la muda mrefu la ukosefu wa masoko rasmi ya madini hususan kwa wachimbaji wadogo. Vilevile, masoko hayo yatarahisisha

upatikanaji wa takwimu sahihi za madini yanayouzwa katika masoko na ukusanyaji wa tozo za Serikali.

### iii. Kudhibiti Utoroshaji wa Madini

117. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kudhibiti utoroshaji wa madini nchini, Wizara itaendelea kuimarisha ulinzi na usimamizi katika maeneo yote ya uzalishaji. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na mamlaka nyingine zenye dhamana ya ulinzi na usalama itaendelea kuhakikisha kuwa katika maeneo ya viwanja vya ndege, bandari na mipakani kunakuwa na usimamizi madhubuti ili kudhibiti utoroshaji wa madini na kuhakikisha kuwa shughuli za madini zinakuwa na manufaa zaidi kwa Watanzania.

### iv. Kuendeleza Wachimbaji Wadogo

118. ***Mheshimiwa Spika,*** katika jitihada za kuwaendeleza wachimbaji wadogo wa madini nchini, Wizara itafanya yafuatayo:- kuendelea kuwapatia maeneo yanayofaa wachimbaji wadogo; kutoa huduma nafuu za kitaalam kwa wachimbaji wadogo ikiwa ni pamoja na kuwafahamisha kuhusu uwepo wa mashapo; kutoa elimu kwa wachimbaji wadogo kuhusu uchimbaji wa madini wenye tija kupitia Vituo vya Umahiri na Vituo vya Mfano vilivojengwa; na kuendelea kuwapatia elimu na kuwakumbusha umuhimu wa kufanya shughuli zao kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na taratibu zinazosimamia Sekta ya Madini.

## v. Kuhamasisha Shughuli za Uongezaji Thamani Madini

119. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuongeza thamani madini, Wizara itahamasisha wawekezaji wa ndani na nje kujenga viwanda vya kuchakata madini hapa nchini kama vile viwanda vya uchenjuaji na uyeyushaji wa madini ya metali *(Smelters & Refineries).* Hii itasaidia kuongeza mapato; ajira kwa Watanzania; na kukuza matumizi ya teknolojia.

## vi. Kuimarisha Ufuatiliaji na Ukaguzi wa Usalama, Afya, Mazingira na Uzalishaji wa Madini katika Migodi

120. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuhakikisha kuwa shughuli za uchimbaji wa madini hapa nchini zinafanyika kwa kuzingatia taratibu za usalama, afya, na utunzaji wa mazingira, Wizara itaendelea kuimarisha na kutekeleza mikakati mbalimbali iliyojiwekea. Mikakati hiyo ni pamoja na:- kufanya kaguzi za mara kwa mara na kufuatilia utekelezaji wa kasoro za kiusalama, afya na mazingira zitakazobainika; kuhakikisha kuwa migodi mikubwa na ya kati inaweka Hati Fungani ya Uhifadhi wa Mazingira *(Environmental Rehabilitation Bond)*; kusimamia Mipango ya Ufungaji Migodi *(Mining Closure Plans)*; kuhakikisha kuwa migodi yote ya uchimbaji mdogo inakuwa na Mpango wa Utunzaji Mazingira *(Environmental Protection Plan - EPP)* na ambayo inakidhi matakwa ya Sheria; kusimamia utekelezaji wa Mkataba wa Minamata wa kupunguza

na kuzuia matumizi ya zebaki katika uchenjuaji kwa kuhamasisha matumizi ya teknolojia rafiki zisizotumia zebaki; kukagua na kuhakiki kiasi na ubora wa madini yanayozalishwa na migodi mikubwa, ya kati na midogo; na kuimarisha ushirikiano na Taasisi nyingine za Serikali zinazohusika na usimamizi wa masuala ya afya, usalama na utunzaji wa mazingira.

### vii. Kuhamasisha Uwekezaji katika Sekta ya Madini

121. ***Mheshimiwa Spika,*** Tanzania ni moja ya nchi iliyobarikiwa kuwa na madini mengi na yenye thamani. Uwepo wa utajiri wa madini haya unatoa fursa mbalimbali za uwekezaji. Fursa hizo zinapatikana katika mnyororo mzima wa madini ambao huhusisha shughuli za utafutaji, uchimbaji, uchenjuaji na biashara ya madini. Katika kuhamasisha na kutangaza fursa hizi, Wizara itaendelea kushirikiana na Balozi zetu zilizopo nchi mbalimbali pamoja na Kituo cha Uwekezaji Tanzania *(TIC)*. Wizara pia itashiriki kwenye makongamano na mikutano mbalimbali inayohusu shughuli za madini ndani na nje ya nchi. Vilevile, Wizara itahakikisha upatikanaji wa taarifa za kijiosayansi kwa wawekezaji.

### viii. Ushiriki wa Watanzania Katika Shughuli za Madini (Local Content)

122. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara itaendelea kusimamia na kuhakikisha kuwa kampuni za uwekezaji katika Sekta ya Madini zinafuata Sheria ya Madini Sura ya

123 ambayo inaelekeza kampuni zote

zinazoomba leseni za utafutaji na uchimbaji wa madini nchini kuwa na mpango wa matumizi ya bidhaa zinazozalishwa na huduma zinazotolewa na watanzania au kampuni za watanzania. Lengo la takwa hilo la kisheria ni kuhakikisha kuwa kampuni hizo zinatumia malighafi na bidhaa zinazozalishwa hapa nchini na huduma mbalimbali zinazotolewa na watanzania pamoja na kampuni za watanzania.

## ix. Kuendeleza Rasilimaliwatu na Kuboresha Mazingira ya Kufanyia Kazi

123. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kutekeleza majukumu iliyojipangia ipasavyo, Wizara itahakikisha inajenga ujuzi wa watumishi kwenye nyanja mbalimbali zikiwemo Uhandisi Migodi, na uongezaji thamani madini ili kuongeza tija na ufanisi katika utendaji kazi wao. Vilevile, Wizara itaboresha mazingira ya kufanyia kazi kwa kununua vitendea kazi mbalimbali pamoja na kuboresha ustawi wa watumishi. Aidha, Wizara itaendelea kutoa elimu juu ya afya bora hususan kwa watumishi wanaoishi na virusi vya ugonjwa wa UKIMWI waliojitokeza. Wizara pia itaendelea kutoa elimu mahali pa kazi ili kuzuia maambukizi mapya ya ugonjwa wa UKIMWI na Magonjwa Sugu Yasiyoambukiza. Aidha, elimu itatolewa kuhusu rushwa na madhara yake katika utendaji wa kazi. Pia, kutokana na upungufu wa watumishi uliopo kwenye kada mbalimbali, Wizara itaendelea kufuatilia Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora ili kupata watumishi zaidi.

124. ***Mheshimiwa Spika,*** sambamba na vipaumbele vya Wizara nilivyovielezea, Wizara itaendelea kutekeleza Mradi wa Usimamizi Endelevu wa Rasilimali Madini (SMMRP) ili kutimiza lengo lake la kuboresha manufaa ya kijamii na kiuchumi yatokanayo na uchimbaji wa madini nchini kwa;- kuimarisha zaidi sehemu ya miradi ya kiuchumi na kijamii na hivyo kuhakikisha ukuaji mkubwa wa maendeleo ya wananchi na Taifa kwa ujumla.

125. ***Mheshimiwa Spika,*** kazi zitakazotekelezwa kupitia Mradi wa SMMRP katika Mwaka 2019/20 ni pamoja na: kujenga uwezo kwa Wizara pamoja na Taasisi zinazohusika katika suala la kupambana na utoroshwaji madini; kuwezesha shughuli za utafiti wa madini ili kuongeza taarifa za kijiolojia na kuvutia uwekezaji; kuwezesha shughuli za uhamasishaji wa uongezaji thamani madini nchini; kuwezesha mapitio na uandaaji wa Mkakati wa Sera ya Madini; na kuijengea uwezo Wizara katika suala la uongozi na uwekaji wazi wa mikataba na umiliki katika shughuli za madini.

## KAZI ZITAKAZOTEKELEZWA NA TAASISI ZILIZO CHINI YA WIZARA KWA MWAKA 2019/20

### i. Tume ya Madini

126. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka 2019/20 Tume ya Madini itatekeleza shughuli zifuatazo: kuimarisha shughuli za ukusanyaji wa mapato ya Serikali yatokanayo na rasilimali madini; kuimarisha ukaguzi wa usalama, afya, mazingira na uzalishaji wa madini katika migodi midogo, ya kati na mikubwa na kusimamia shughuli za uzalishaji katika mitambo ya

uchenjuaji wa madini; kuendelea kuboresha mazingira ya kuwawezesha wananchi kunufaika na rasilimali madini; kuimarisha udhibiti wa utoroshwaji wa madini; kuimarisha usimamizi wa biashara ya madini na kushughulikia migogoro inayotokana na shughuli za madini.

127. ***Mheshimiwa Spika,*** Tume ya Madini pia itaboresha Mfumo wa kielektroniki wa kutoa na kusimamia taarifa za leseni za madini ili kuondoa migogoro inayotokana na leseni; itaimarisha shughuli za uongezaji thamani madini; itaelimisha Umma na kuboresha mawasiliano kati ya Tume na wadau mbalimbali kuhusu Sheria, Kanuni na Taratibu zinazosimamia Sekta ya Madini; na itaendeleza rasilimaliwatu na kuboresha mazingira ya kufanyia kazi.

### ii. Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini Tanzania (GST)

128. ***Mheshimiwa Spika,*** kazi zilizopangwa kutekelezwa na GST katika Mwaka 2019/20 ni pamoja na kuboresha Kanzidata ya Taifa ya taarifa za jiosayansi na Madini ili kuongeza uelewa wa jiolojia ya nchi na kuchochea uwekezaji katika Sekta ya Madini nchini; kuwaendeleza wachimbaji wadogo kwa kufanya tafiti za jiosayansi katika utafutaji, uchimbaji salama, uhifadhi wa mazingira na uchenjuaji ili kuongeza tija katika uzalishaji; kukusanya na kuhakiki taarifa za utafutaji na uchimbaji madini kutoka kwa wamiliki wa leseni ili kubaini uhalisia wake *(authenticity)*; kuboresha huduma za maabara kwa wadau wa Sekta ya Madini, Kilimo na Ujenzi;

kuboresha kanzidata ya majanga asilia ya jiolojia na kuelimisha wananchi namna bora ya kujikinga na majanga hayo; kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya GST kutoka katika vyanzo vyake mbalimbali; na kuendeleza rasilimaliwatu na kuboresha mazingira ya kufanyia kazi.

### iii. Shirika la Madini la Taifa (STAMICO)

129. ***Mheshimiwa Spika,*** STAMICO inatarajia kutekeleza kazi zifuatazo katika Mwaka 2019/20: kuendeleza uchimbaji na uuzaji wa makaa ya mawe katika eneo la Kabulo sanjari na kuanza uzalishaji wa nishati mbadala za kupikia *(coal briquette)*; kuendeleza Mradi wa dhahabu wa Buhemba kwa kuanza uchenjuaji wa mabaki ya mchanga wa dhahabu katika eneo la mradi; kuanzisha Mradi wa uchimbaji na uuzaji wa kokoto wa Chigongwe (Dodoma); kuimarisha usimamizi wa miradi ya ubia (TanzaniteOne na Bukreef) na kampuni ya STAMIGOLD; kuimarisha biashara ya shughuli za uchorongaji na utoaji wa ushauri wa kitaalam katika Sekta ya Madini; na kuratibu uboreshaji na uendelezaji wa shughuli za wachimbaji wadogo nchini.

### iv. Taasisi ya Uhamasishaji Uwazi na Uwajibikaji katika Rasilimali Madini, Mafuta na Gesi Asilia (TEITI)

130. ***Mheshimiwa Spika,*** kazi zitakazotekelezwa na TEITI katika Mwaka 2019/20 zitahusisha: kukamilisha na kutoa kwa umma Ripoti ya Malipo ya Kodi yanayofanywa na Kampuni za Madini, Mafuta na

Gesi Asilia kwa Serikali kwa kipindi cha 2017/18 na 2018/19; kuendelea kuelimisha Umma kwa njia ya warsha, matangazo, vipindi vya redio, televisheni na makala kuhusu matumizi ya takwimu zinazotolewa katika ripoti za TEITI ili waweze kutumia takwimu hizo katika kuhoji uwajibikaji wa Serikali; kukamilisha uwekaji wazi kwa Umma Mikataba ya Kampuni za Madini, Mafuta na Gesi Asilia *(MDAs and PSAs)*; na kukamilisha uanzishwaji wa rejista ya taarifa na majina ya watu wanaomiliki hisa katika Kampuni za Madini, Mafuta na Gesi Asilia ili kupunguza mianya ya rushwa na ukwepaji wa kodi.

### v. Chuo cha Madini (MRI)

*131.* ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka 2019/20 Chuo cha Madini kinatarajia kuendelea kutoa mafunzo kwa wanafunzi ambapo kitadahili jumla ya wanafunzi **710**; kuendelea kuboresha miundombinu ya Chuo ikiwa ni pamoja na uendelezaji wa Kampasi ya Nzega; kuendelea kufanya tafiti na kutoa ushauri wa kitaalam; na kujenga uwezo wa watumishi.

### vi. Kituo cha Jemolojia Tanzania (TGC)

132. ***Mheshimiwa Spika,*** Kituo cha Jemolojia Tanzania pamoja na majukumu mengine kina dhamana ya kutoa mafunzo ya uongezaji thamani madini ya vito. Katika Mwaka 2019/20, kama ilivyoainishwa katika Mpango Mkakati wa Biashara kituo kimepanga kutekeleza yafuatayo: kutoa mafunzo ya muda mrefu ngazi ya stashahada; kuendesha mafunzo ya muda mfupi kwenye fani za uchongaji wa vinyango na miamba *(carving)*, elimu ya

madini ya vito *(Gemology)*, ukataji na ung'arishaji madini ya vito *(lapidary)* na usonara; utengenezaji wa bidhaa kwa kutumia miamba na madini ya vito na kushirikiana na taasisi za nje zilizobobea kwenye fani ya uongezaji thamani madini kwa ajili ya kujiimarisha na kujijengea uwezo.

## D. SHUKRANI

133. ***Mheshimiwa Spika,*** mafanikio yaliyofikiwa katika kuendeleza Sekta ya Madini yanatokana na michango inayoendelea kutolewa na wadau mbalimbali. Kipekee nimshukuru Mheshimiwa Stanslaus Haroon Nyongo Mbunge na Naibu Waziri Madini kwa namna anavyonipa ushirikiano katika kusimamia Sekta ya Madini. Hakika nikiri kuwa tangu tulivyochaguliwa wote kama Manaibu Waziri wa Wizara hii, na kwa sasa akiwa kama Naibu wangu, amekuwa na mchango mkubwa katika kusimamia Sekta hii.

134. ***Mheshimiwa Spika,*** nipende pia kumshukuru Prof. Simon Samwel Msanjila, Katibu Mkuu wa Wizara ya Madini kwa namna anavyosimamia utekelezaji wa majukumu ya Wizara. Aidha, niwashukuru Mwenyekiti wa Tume ya Madini Prof. Kikula, Katibu Mtendaji wa Tume ya Madini Prof. Shukrani Manya na Makamishina wote wa Tume kwa kusimamia kwa umakini uendeshaji wa Tume. Kipekee, nawashukuru Wakuu wa Idara na Vitengo; Wenyeviti wa Bodi zilizo chini ya Wizara; Viongozi wa Taasisi na Wafanyakazi wote wa Wizara na Taasisi zake kwa ushirikiano mkubwa wanaonipatia pamoja na kujituma kwao katika kuhakikisha kuwa majukumu ya Wizara ya Madini yanatimizwa ipasavyo

na hivyo kuifanya Sekta ya Madini kuwa chachu ya maendeleo.

135. ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, naomba nitumie fursa hii kuwashukuru washirika wetu wote wa maendeleo ambao wamekuwa bega kwa bega na Wizara katika utekelezaji wa mipango yetu ya Sekta ya Madini. Washirika hao wa maendeleo wanajumuisha: Benki ya Dunia; Serikali za Jamhuri ya Watu wa China, Jamhuri ya Watu wa Korea ya Kusini, Misri, na Australia. Serikali itaendelea kushirikiana na washirika hao na wengine katika kuendeleza Sekta ya Madini nchini.

136. ***Mheshimiwa Spika,*** naomba kutoa shukrani zangu za pekee na za dhati kwa wananchi wa jimbo la Bukombe ambao kwa muda wote wameendelea kuniamini na kunipa ushirikiano katika kutekeleza majukumu yangu ya kijimbo na kitaifa. Napenda kuwahaidi na kuwahakikishia kuwa nitaendelea kuwatumikia kwa nguvu zangu zote na kipaji nilichopewa na mwenyezi Mungu katika kuleta maendeleo ya Jimbo letu na Taifa kwa ujumla.

137. ***Mheshimiwa Spika,*** nitakuwa mchoyo wa fadhila kama sitamshukuru kwa dhati mke wangu mpenzi Benadetha Clement Mathayo pamoja na watoto wangu Elshadai, Elvin, Elis, Abigael, Amon, Abishai na Moses kwa kunivumilia, kuniunga mkono na kuniombea kwa Mwenyezi Mungu ili niweze kutekeleza majukumu niliyopewa na Mheshimiwa Rais katika kujenga na kutetea maslahi ya Taifa letu.

## E. HITIMISHO

138. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kutekeleza majukumu ya Wizara ya Madini katika Mwaka 2019/20, naomba Bunge lako Tukufu sasa liridhie na kupitisha makadirio ya Jumla ya **shilingi 49,466,898,200** kwa ajili ya Matumizi ya Wizara na Taasisi zake kwa Mwaka 2019/20. Mchanganuo wa Bajeti hiyo ni kama ifuatavyo:-

(i) Bajeti ya Maendeleo ni **shilingi 7,039,810,200** ambazo zote ni fedha za ndani; na

*(ii)* Bajeti ya Matumizi ya Kawaida ni **shilingi 42,427,088,000,** ambapo **shilingi 16,473,825,000** ni kwa ajili ya Mishahara na **shilingi 25,953,263,000** ni Matumizi Mengineyo *(OC).*

139. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mara nyingine tena naomba kutoa shukrani zangu za dhati kwako wewe binafsi, Naibu Spika, Wenyeviti wa Bunge na kwa Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza. Hotuba hii pia inapatikana katika Tovuti ya Wizara kwa anuani ya www.madini.go.tz.

140. ***Mheshimiwa Spika,*** naomba kutoa hoja.

## VIAMBATISHO

# VIELELEZO VYA HOTUBA YA BAJETI YA WIZARA YA MADINI KWA MWAKA 2018/19

***Jedwali Na. 1:*** *Makadirio na Makusanyo Halisi ya Maduhuli kwa Kila Kituo kwa Mwaka 2018/19 pamoja na Makadirio kwa Mwaka 2019/20*

| Na. | MKOA / KITUO CHA MAKUSANYO | Malengo ya Makusanyo kwa Mwaka2018/19 | Makusanyo halisi kufikia Machi, 2019 | Asilimia ya Makusanyo kwa Mwaka 2018/19 | Malengo ya Makusanyo kwa Mwaka 2019/20 |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Dodoma - Makao Makuu | 25,000,000,000 | 13,627,206,619 | 55 | 26,049,500,000 |
| 2 | Ofisi ya Madini-Simiyu | 200,000,000 | 46,036,293 | 23 | 200,000,000 |
| 3 | Ofisi ya Madini-Kagera | 2,500,000,000 | 1,663,594,235 | 67 | 3,500,000,000 |
| 4 | Ofisi ya Madini-Songwe | 8,600,000,000 | 7,167,360,564 | 83 | 18,860,500,000 |
| 5 | Ofisi ya Madini-Dodoma | 1,500,000,000 | 1,219,567,325 | 81 | 2,800,000,000 |
| 6 | Ofisi ya Madini-Geita | 90,000,000,000 | 98,114,478,385 | 109 | 155,849,687,500 |
| 7 | Ofisi ya Madini-Kahama | 50,000,000,000 | 28,288,393,206 | 57 | 78,785,000,000 |
| 8 | Ofisi ya Madini-Kigoma | 820,004,000 | 252,698,345 | 31 | 1,000,000,000 |
| 9 | Ofisi ya Madini-Mirelani | 2,500,000,000 | 1,776,122,824 | 71 | 6,389,250,000 |
| 10 | Ofisi ya Madini-Morogoro | 1,500,000,000 | 799,075,303 | 53 | 2,200,000,000 |
| 11 | Ofisi ya Madini-Kilimanjar | 1,500,000,000 | 781,776,772 | 52 | 2,000,000,000 |
| 12 | Ofisi ya Madini-Mara | 70,000,000,000 | 50,497,444,162 | 72 | 103,099,000,000 |
| 13 | Ofisi ya Madini-Lindi | 1,500,000,000 | 867,726,673 | 58 | 2,000,000,000 |
| 14 | Ofisi ya Madini-Njombe | 1,000,000,000 | 385,393,425 | 39 | 1,515,700,000 |
| 15 | Ofisi ya Madini-Tabora | 1,500,000,000 | 736,878,940 | 49 | 2,273,550,000 |
| 16 | Ofisi ya Madini-Tanga | 3,500,000,000 | 1,836,349,192 | 52 | 4,300,000,000 |
| 17 | Ofisi ya Madini-Arusha | 2,400,000,000 | 1,862,568,642 | 78 | 3,789,250,000 |
| 18 | Ofisi ya Madini-Mbeya | 14,875,000,000 | 9,910,980,758 | 67 | 8,875,000,000 |
| 19 | Ofisi ya Madini-Katavi | 975,000,000 | 471,323,626 | 48 | 1,000,000,000 |
| 20 | Ofisi ya Madini-Mtwara | 2,500,000,000 | 1,174,804,942 | 47 | 3,010,000,000 |
| 21 | Ofisi ya Madini-Mwanza | 2,500,000,000 | 1,369,164,485 | 55 | 3,000,000,000 |
| 22 | Ofisi ya Madini-DSM | 8,000,000,000 | 5,553,900,816 | 69 | 13,157,000,000 |
| 23 | Ofisi ya Madini-Shinyanga | 12,000,000,000 | 11,100,679,727 | 93 | 18,157,000,000 |
| 24 | Ofisi ya Madini-Singida | 1,000,000,000 | 457,734,284 | 46 | 1,500,000,000 |
| 25 | Ofisi ya Madini-Ruvuma | 4,200,000,000 | 3,867,650,298 | 92 | 5,043,960,000 |
| 26 | Ofisi ya Madini-Rukwa | 150,000,000 | 110,154,903 | 73 | 1,000,000,000 |
| 27 | Ofisi ya Madini-Manyara | 100,000,000 | 67,951,951 | 68 | 1,000,000,000 |
| **JUMLA** | | **310,320,004,000** | **244,007,016,694** | **79** | **470,354,397,500** |

***Chanzo:*** *Tume ya Madini, 2019*

***Jedwali Na. 2:*** *Takwimu za Mitambo ya Uchenjuaji Dhahabu (Elutions) Nchini*

| Na | Mkoa | Mahali | Inayofanya Kazi | Iliyosimama | Hatuaya Ujenzi | Hatua za Majaribio | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Mara | Musoma | 13 | - | 2 | - | 15 |
| | | Tarime | 2 | - | 1 | - | 3 |
| 2 | Kahama | Kahama | 11 | 02 | 01 | 02 | 16 |
| 3 | Geita | Geita | 33 | - | - | - | 33 |
| 4 | Dodoma | Dodoma | 2 | 1 | - | - | 3 |
| 5 | Lindi | Lindi | 1 | - | - | - | 1 |
| 6 | Tabora | Tabora | 5 | 1 | - | - | 6 |
| 7 | Mbeya | Mbeya | 0 | 4 | 0 | 0 | 4 |
| 8 | Shinyanga | Shinyanga | 3 | 3 | - | - | 6 |
| 9 | Mwanza | Mwanza | 5 | - | 1 | - | 6 |
| 10 | Iringa | Iringa | 2 | - | - | - | 2 |
| **Jumla** | | | **77** | **11** | **5** | **2** | **95** |

**Chanzo:** *Tume ya Madini, 2019*

**Jedwali Na. 3:** *Kiasi cha Mrabaha na ada ya ukaguzi kilichokusanywa kutoka kwenye madini mbalimbali kuanzia mwezi Julai, 2018 hadi Machi, 2019*

| Na | Aina ya Madini | Kipimo cha Uzito | Uzito | Thamani (TZS) | Mrabaha (TZS) | Ada ya Ukaguzi (TZS) | Makusanyo (TZS) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Dhahabu (SMLs na MLs) | Kg | 27,550.91 | 2,522,921,796,902.50 | 151,375,307,814.15 | 25,229,217,969.03 | 176,604,525,783.18 |
| 2 | Dhahabu (PMLs, PCLs na Dealers) | Kg | 2,214.99 | 201,856,812,436.93 | 12,111,408,746.22 | 2,018,568,124.37 | 14,129,976,870.58 |
| 3 | Fedha (Silver) | Kg | 9,406.88 | 10,657,002,819.71 | 639,420,169.18 | 106,570,028.20 | 745,990,197.38 |
| 4 | Almasi (WDL) | Karati | 309,303.85 | 161,105,379,136.69 | 9,666,322,748.20 | 1,611,053,791.37 | 11,277,376,539.57 |
| 5 | Almasi (El Hillal) | Karati | 3,352.90 | 1,746,406,408.16 | 104,784,384.49 | 17,464,064.08 | 122,248,448.57 |
| 6 | Almasi (Dealers) | Karati | 4,747.45 | 2,472,777,924.30 | 148,366,675.46 | 24,727,779.24 | 173,094,454.70 |
| 7 | Tanzanite (ghafi) | Kg | 768.75 | 14,031,547,691.59 | 841,892,861.50 | 140,315,476.92 | 982,208,338.41 |
| 8 | Tanzanite (Cut and Polished) | Ct | 87,389.02 | 6,698,067,975.79 | 66,980,679.76 | 66,980,679.76 | 133,961,359.52 |
| 9 | Tanzanite (Magonga) | Kg | 13,146.07 | 623,375,446.77 | 37,402,526.81 | 6,233,754.47 | 43,636,281.27 |
| 10 | Madini ya Kinywe (Graphite) | Tani | 9,127.94 | 10,142,189,518.46 | 304,265,685.55 | 101,421,895.18 | 405,687,580.74 |
| 11 | Makaa ya Mawe (Ngaka) | Tani | 603,325.11 | 68,720,466,195.67 | 2,061,613,985.87 | 687,204,661.96 | 2,748,818,647.83 |
| 12 | Makaa ya Mawe (Kabulo) | Tani | 7,370.69 | 839,542,801.37 | 25,186,284.04 | 8,395,428.01 | 33,581,712.05 |
| 13 | Makaa ya Mawe (Sumbawanga) | Tani | 7,696.96 | 876,705,893.26 | 26,301,176.80 | 8,767,058.93 | 35,068,235.73 |
| 14 | Madini mengine ya Vito | Kg | 534,728.48 | 18,923,793,281.74 | 1,133,664,385.62 | 189,237,932.82 | 1,322,902,318.44 |
| 15 | Madini ya Ujenzi | Tani | 13,087,435.48 | 226,715,242,680.80 | 6,801,457,280.42 | 1,996,691,511.91 | 8,798,148,792.33 |
| 16 | Madini ya Viwandani | Tani | 5,351,227.42 | 118,995,927,877.03 | 3,577,870,452.03 | 1,174,637,572.10 | 4,752,508,024.13 |
| 17 | Madini Mengineyo | Tani | 720,429.47 | 30,347,668,089.53 | 910,430,042.69 | 303,476,681.18 | 1,213,906,723.86 |
| | **Jumla** | | | **3,397,674,703,080.28** | **189,832,675,898.78** | **33,690,964,409.52** | **223,523,640,308.30** |

***Chanzo:*** *Tume ya Madini, 2019*

***Jedwali Na.4:*** *Kiasi na Thamani ya Madini yaliyouzwa Nje ya Nchi kuanzia Mwaka 2013 - 2018*

| Aina ya Madini | Kipimo | Kiasi kilichouzwa | | | | | | Thamani ('000 "US$) | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 2013 | 2014 | 2015 | 2016 | 2017 | 2018 | 2013 | 2014 | 2015 | 2016 | 2017 | 2018 |
| Almasi (Rough) | 000 Carats | 179,633.00 | 252,875.00 | 216,491.00 | 239,305.00 | 304,456.00 | 383,391.15 | 46,013.00 | 82,053.00 | 56,003.00 | 85,090.00 | 67,510.00 | 96,066.00 |
| Dhahabu | 000 Gramu | 42,534.00 | 40,481.00 | 43,358.00 | 45,155.00 | 43,490.00 | 35,797.85 | 1,735,708.00 | 1,640,072.00 | 1,609,392.00 | 1,824,815.00 | 1,636,575.00 | 1,452,850.00 |
| Gemstones | 000 Gramu | 1,086,532.00 | 3,083,765.00 | 1,872,915.00 | 2,944,107.00 | 1,185,697.00 | 284,321.19 | 62,453.00 | 49,146.00 | 46,067.00 | 60,483.00 | 53,596.00 | 28,006.00 |
| Chumvi | Tani | 33,210.00 | 54,757.00 | 92,158.00 | 145,718.00 | 100,017.00 | 36,392.41 | 3,785.00 | 5,275.00 | 5,071.00 | 4,806.00 | 3,803.00 | 1,207.00 |
| Phosphate | Tani | 397,020.00 | 738,000.00 | 222,800.00 | 23,658.00 | 1,351.00 | - | 225.00 | 140.00 | 126.00 | 721.00 | 585.00 | - |
| Bati | Tani | - | 79.00 | 179.00 | 138.00 | 91.00 | 8.04 | - | 907.00 | 959.00 | 1,499.00 | 1,037.00 | - |
| Jasi | Tani | - | 200,179.00 | 235,920.00 | 213,744.00 | 123,645.00 | - | 231.00 | 2,518.00 | 4,445.00 | 6,279.00 | 3,187.00 | - |
| Graphite | Tani | - | 25.00 | 30.00 | 1,180.00 | 128.00 | 27,810.00 | - | 3.00 | 5.00 | 2,132.00 | 18.00 | 2,417.77 |
| Fedha | 000 Gramu | 11,013.00 | 14,493.00 | 15,569.00 | 17,984.00 | 10,911.00 | 12,114.04 | 17,214.00 | 10,283.00 | 7,626.00 | 9,901.00 | 5,850.00 | 6,075.00 |
| Shaba | 000 Lb | 12,654.00 | 14,027.00 | 14,252.00 | 16,247.00 | 2,934.00 | - | 42,134.00 | 43,675.00 | 35,658.00 | 35,421.00 | 7,741.00 | - |
| Madini ya Viwanda | Tani | - | 98.00 | 151,297.00 | 4,769,577.00 | 708,047.00 | 783,180.00 | - | 9.00 | 3,254.00 | 78,491.00 | 29,896.00 | 35,783.00 |
| Bauxite | Tani | 39,977,300.00 | 25,641,201.00 | 204,956.00 | 74,660.00 | 12,090.00 | 7,140.20 | 35,827.00 | 20,014.00 | 325.00 | 1,242.00 | 898.00 | 335.12 |
| **Jumla ('000 US$)** | | | | | | | | **1,943,590.00** | **1,854,095.00** | **1,768,931.00** | **2,110,880.00** | **1,810,696.00** | **1,622,739.90** |

***Chanzo:*** *Tume ya Madini, 2019*

***Jedwali Na. 5:*** *Matukio ya Matetemeko ya ardhi katika maeneo mbalimbali ya Tanzania kuanzia mwezi Julai, 2018 – Machi, 2019*

| S/N | Tarehe | Muda | Kipimo (Richter Scale) | Sehemu | | | DEPTH (KM) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | Eneo lilipotokea | LATITUDE (S ) | LONGITUDE ( E) | |
| 1 | 05/08/2018 | 07:58:27 Mchana | 4.5 | Arusha | -2.9203 | 35.5791 | 14.39 |
| 2 | 06/8/2018 | 06:07:47 Usiku | 4.4 | Lake Tanganyika Region | -7.5473 | 30.4413 | 10.0 |
| 3 | 08/08/2018 | 06:07:22 Usiku | 4.2 | Manyara | -3.7282 | 35.6252 | 10.0 |
| 4 | 08/08/2018 | 06:07:47 Usiku | 4.4 | Lake Tanganyika Region | -7.49 | 30.42 | 10.0 |
| 5 | 16/08/2018 | 06:09:27 Usiku | 4.2 | Iringa | -7.3569 | 34.9152 | |
| 6 | 22/08/2018 | 02:30:34 Asubuhi | 4.6 | Singida | -4.7883 | 34.9369 | 10.0 |
| 7 | 26/08/2018 | 05:46:41 Usiku | 4.7 | Lake Tanganyika Region | -6.4235 | 30.9612 | 10.0 |
| 8 | 24/11/2018 | 05:05:17 Usiku | 4.2 | Lake Tanganyika Region | -6.5347 | 31.0329 | 10 |
| 9 | 25/12/2018 | 04:22:16 Usiku | 1.2 | Nala/Dodoma | -6.070790 | 35.667062 | 15.0 |
| 10 | 25/12/2018 | 01:10:00 Usiku | 2.3 | Nala/Dodoma | -6.076535 | 35.655136 | 15.0 |
| 11 | 27/12/2018 | 04:37:54Jioni | 2.9 | Nala/Dodoma | -6.612098 | 35.618488 | 15.0 |
| 12 | 01/01/2019 | 04:12:52 Usiku | 2.6 | Nala/Dodoma | -6.048769 | 35.711324 | 15.0 |
| 13 | 01/01/2019 | 03:02:53 Usiku | 1.5 | Nala/Dodoma | -6.050221 | 35.740005 | 15.0 |
| 14 | 01/01/2019 | 04:25:04 Usiku | 2.5 | Nala/Dodoma | -6.052410 | 35.703603 | 15.0 |
| 15 | 01/01/2019 | 03:06:25 Usiku | 2.8 | Nala/Dodoma | -6.052899 | 35.705009 | 15.0 |
| 16 | 01/01/2019 | 02:19:23 Usiku | 1.7 | Nala/Dodoma | -6.054793 | 35.694677 | 15.0 |
| 17 | 01/01/2019 | 04:06:25 Usiku | 1.5 | Nala/Dodoma | -6.055315 | 35.693503 | 15.0 |
| 18 | 01/01/2019 | 04:50:50 Asubuhi | 2.5 | Nala/Dodoma | -6.055884 | 35.675693 | 15.0 |

| S/N | Tarehe | Muda | Kipimo (Richter Scale) | Sehemu | | | DEPTH (KM) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | Eneo lilipotokea | LATITUDE (S ) | LONGITUDE ( E) | |
| 19 | 01/01/2019 | 02:26:52 Asubuhi | 3.5 | Nala/Dodoma | -6.056258 | 35.686813 | 15.0 |
| 20 | 01/01/2019 | 06:41:16 Mchana | 3.6 | Nala/Dodoma | -6.057331 | 35.682561 | 15.0 |
| 21 | 01/01/2019 | 11:39:13 Jioni | 2.5 | Nala/Dodoma | -6.058270 | 35.675207 | 15.0 |
| 22 | 01/01/2019 | 06:49:10 Usiku | 2.2 | Nala/Dodoma | -6.059021 | 35.683147 | 15.0 |
| 23 | 01/01/2019 | 04:52:01 Usiku | 1.8 | Nala/Dodoma | -6.059967 | 35.681379 | 15.0 |
| 24 | 01/01/2019 | 02:39:13 Usiku | 3.5 | Nala/Dodoma | -6.060618 | 35.678329 | 15.0 |
| 25 | 01/01/2019 | 07:07:33 Mchana | 2.8 | Nala/Dodoma | -6.060650 | 35.682040 | 15.0 |
| 26 | 01/01/2019 | 06:35:12 Mchana | 1.4 | Nala/Dodoma | -6.060912 | 35.682059 | 15.0 |
| 27 | 01/01/2019 | 12:18:40 Jioni | 3.3 | Nala/Dodoma | -6.061577 | 35.674790 | 15.0 |
| 28 | 01/01/2019 | 05:35:22 Asubuhi | 2.3 | Nala/Dodoma | -6.061845 | 35.674376 | 15.0 |
| 29 | 01/01/2019 | 06:02:09 Mchana | 3.3 | Nala/Dodoma | -6.062193 | 35.675453 | 15.0 |
| 30 | 01/01/2019 | 07:10:52 Mchana | 1.8 | Nala/Dodoma | -6.063283 | 35.670182 | 15.0 |
| 31 | 01/01/2019 | 12:53:25 Jioni | 2.7 | Nala/Dodoma | -6.063699 | 35.678310 | 15.0 |
| 32 | 01/01/2019 | 05:33:01 Asubuhi | 0.4 | Nala/Dodoma | -6.063861 | 35.676429 | 15.0 |
| 33 | 01/01/2019 | 02:22:21Usiku | 3.1 | Nala/Dodoma | -6.064740 | 35.661542 | 15.0 |
| 34 | 01/01/2019 | 04:41:39 Asubuhi | 1.3 | Nala/Dodoma | -6.065563 | 35.675145 | 15.0 |
| 35 | 01/01/2019 | 06:18:36 Mchana | 1.7 | Nala/Dodoma | -6.065623 | 35.671669 | 15.0 |
| 36 | 01/01/2019 | 04:57:49Usiku | 1.6 | Nala/Dodoma | -6.066002 | 35.667750 | 15.0 |
| 37 | 01/01/2019 | 11:11:45Jioni | 4.1 | Nala/Dodoma | -6.066855 | 35.657271 | 15.0 |
| 38 | 01/01/2019 | 02:47:49 Usiku | 2.5 | Nala/Dodoma | -6.067274 | 35.665809 | 15.0 |
| 39 | 01/01/2019 | 08:00:06 Mchana | 2.4 | Nala/Dodoma | -6.067676 | 35.662051 | 15.0 |

| S/N | Tarehe | Muda | Kipimo (Richter Scale) | Sehemu | | | DEPTH (KM) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | Eneo lilipotokea | LATITUDE (S ) | LONGITUDE ( E) | |
| 40 | 01/01/2019 | 09:30:15 Mchana | 2.0 | Nala/Dodoma | -6.067835 | 35.678437 | 15.0 |
| 41 | 01/01/2019 | 03:53:28 Asubuhi | 3.0 | Nala/Dodoma | -6.067855 | 35.666525 | 15.0 |
| 42 | 01/01/2019 | 03:36:58 Asubuhi | 3.8 | Nala/Dodoma | -6.067871 | 35.666551 | 15.0 |
| 43 | 01/01/2019 | 06:42:14 Mchana | 2.4 | Nala/Dodoma | -6.068080 | 35.671161 | 15.0 |
| 44 | 01/01/2019 | 09:35:46 Jioni | 2.6 | Nala/Dodoma | -6.068296 | 35.66175 | 15.0 |
| 45 | 01/01/2019 | 04:24:41 Asubuhi | 1.6 | Nala/Dodoma | 6.068567° | 35.663944 | 15.0 |
| 46 | 01/01/2019 | 02:26:01 Usiku | 1.9 | Nala/Dodoma | -6.070175 | 35.658813 | 15.0 |
| 47 | 01/01/2019 | 11:04:47 Jioni | 1.6 | Nala/Dodoma | -6.071318 | 35.660535 | 15.0 |
| 48 | 01/01/2019 | 06:07:10 Mchana | 3.6 | Nala/Dodoma | -6.071395 | 35.661632 | 15.0 |
| 49 | 01/01/2019 | 04:05:14 Asubuhi | 1.9 | Nala/Dodoma | -6.071456 | 35.660128 | 15.0 |
| 50 | 01/01/2019 | 08:18:46 Mchana | 2.2 | Nala/Dodoma | -6.071606 | 35.659895 | 15.0 |
| 51 | 01/01/2019 | 02:10:19 Usiku | 2.6 | Nala/Dodoma | -6.071831 | 35.661046 | 15.0 |
| 52 | 01/01/2019 | 06:20:48 Usiku | 1.0 | Nala/Dodoma | -6.072673 | 35.658487 | 15.0 |
| 53 | 01/01/2019 | 06:24:46 Mchana | 2.7 | Nala/Dodoma | -6.073177 | 35.654990 | 15.0 |
| 54 | 01/01/2019 | 03:38:15 Asubuhi | 3.0 | Nala/Dodoma | -6.073364 | 35.659054 | 15.0 |
| 55 | 01/01/2019 | 07:20:15 Mchana | 2.2 | Nala/Dodoma | -6.073600 | 35.661747 | 15.0 |
| 56 | 01/01/2019 | 07:01:24 Mchana | 2.2 | Nala/Dodoma | -6.074267 | 35.659424 | 15.0 |
| 57 | 01/01/2019 | 11:44:03 Asubuhi | 2.4 | Nala/Dodoma | -6.074281 | 35.659382 | 15.0 |
| 58 | 01/01/2019 | 03:51:40 Asubuhi | 4.9 | Nala/Dodoma | -6.074432 | 35.659231 | 15.0 |
| 59 | 01/01/2019 | 03:14:36 Asubuhi | 4.7 | Nala/Dodoma | -6.074499 | 35.662099 | 15.0 |
| 60 | 01/01/2019 | 04:09:27 Asubuhi | 3.0 | Nala/Dodoma | -6.075425 | 35.659376 | 15.0 |
| 61 | 01/01/2019 | 12:02:50 Jioni | 1.7 | Nala/Dodoma | -6.076368 | 35.654023 | 15.0 |


| S/N | Tarehe | Muda | Kipimo (Richter Scale) | Sehemu | | | DEPTH (KM) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | Eneo lilipotokea | LATITUDE (S ) | LONGITUDE ( E) | |
| 62 | 01/01/2019 | 03:37:08 Asubuhi | 2.7 | Nala/Dodoma | -6.076393 | 35.654019 | 15.0 |
| 63 | 01/01/2019 | 11:16:03 Asubuhi | 2.0 | Nala/Dodoma | -6.076631 | 35.656766 | 15.0 |
| 64 | 01/01/2019 | 02:33:49 Usiku | 3.2 | Nala/Dodoma | -6.076718 | 35.654964 | 15.0 |
| 65 | 01/01/2019 | 04:38:54 Asubuhi | 2.4 | Nala/Dodoma | -6.077293 | 35.657061 | 15.0 |
| 66 | 01/01/2019 | 12:47:36 Jioni | 1.5 | Nala/Dodoma | -6.077509 | 35.652688 | 15.0 |
| 67 | 01/01/2019 | 07:15:15 Usiku | 1.5 | Nala/Dodoma | -6.078208 | 35.651950 | 15.0 |
| 68 | 01/01/2019 | 04:50:23 Asubuhi | 1.8 | Nala/Dodoma | -6.082536 | 35.651126 | 15.0 |
| 69 | 01/01/2019 | 09:48:17 Jioni | 2.9 | Nala/Dodoma | -6.083541 | 35.647781 | 15.0 |
| 70 | 01/01/2019 | 03:30:38 Asubuhi | 3.8 | Nala/Dodoma | 6.085164 | 35.644611 | 15.0 |
| 71 | 01/01/2019 | 04:25:04 Usiku | 1.9 | Nala/Dodoma | -6.090451 | 35.684342 | 15.0 |
| 72 | 01/01/2019 | 11:29:32 Jioni | 1.5 | Nala/Dodoma | -6.090496 | 35.639637 | 15.0 |
| 73 | 01/01/2019 | 11:31:09 Jioni | 2.5 | Nala/Dodoma | -6.091345 | 35.637835 | 15.0 |
| 74 | 01/01/2019 | 06:04:23 Usiku | 1.0 | Nala/Dodoma | -6.093790 | 35.640335 | 15.0 |
| 75 | 01/01/2019 | 05:36:50 Usiku | 1.9 | Nala/Dodoma | -6.110724 | 35.624658 | 15.0 |
| 76 | 02/01/2019 | 07:06:39 Mchana | 1.7 | Nala/Dodoma | -6.052677 | 35.709036 | 15.0 |
| 77 | 02/01/2019 | 06:01:14 Usiku | 0.7 | Nala/Dodoma | -6.053639 | 35.783128 | 15.0 |
| 78 | 02/01/2019 | 06:59:20 Mchana | 1.5 | Nala/Dodoma | -6.055303 | 35.695923 | 15.0 |
| 79 | 02/01/2019 | 07:43:32 Mchana | 2.7 | Nala/Dodoma | -6.055582 | 35.708636 | 15.0 |
| 80 | 02/01/2019 | 02:22:24 Asubuhi | 1.8 | Nala/Dodoma | -6.056529 | 35.695339 | 15.0 |
| 81 | 02/01/2019 | 06:55:06 Mchana | 1.7 | Nala/Dodoma | -6.058669 | 35.686035 | 15.0 |
| 82 | 02/01/2019 | 06:41:44 Mchana | 2.6 | Nala/Dodoma | -6.059927 | 35.675893 | 15.0 |
| 83 | 02/01/2019 | 07:20:15 Mchana | 1.8 | Nala/Dodoma | -6.060506 | 35.678538 | 15.0 |

| S/N | Tarehe | Muda | Kipimo (Richter Scale) | Sehemu | | | DEPTH (KM) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | Eneo lilipotokea | LATITUDE (S ) | LONGITUDE ( E) | |
| 84 | 02/01/2019 | 02:56:02 Asubuhi | 1.9 | Nala/Dodoma | -6.063967 | 35.667605 | 15.0 |
| 85 | 02/01/2019 | 06:11:28 Mchana | 1.1 | Nala/Dodoma | -6.064503 | 35.678776 | 15.0 |
| 86 | 02/01/2019 | 02:56:02 Asubuhi | 1.7 | Nala/Dodoma | -6.065442 | 35.668553 | 15.0 |
| 87 | 02/01/2019 | 03:58:46 Asubuhi | 0.5 | Nala/Dodoma | -6.066019 | 35.669239 | 15.0 |
| 88 | 02/01/2019 | 07:10:52 Mchana | 1.8 | Nala/Dodoma | -6.066325 | 35.675589 | 15.0 |
| 89 | 02/01/2019 | 04:55:28 Usiku | 1.4 | Nala/Dodoma | -6.066352 | 35.672127 | 15.0 |
| 90 | 02/01/2019 | 12:04:35 Jioni | 2.0 | Nala/Dodoma | -6.066434 | 35.670406 | 15.0 |
| 91 | 02/01/2019 | 06:42:14 Mchana | 2.9 | Nala/Dodoma | -6.067268 | 35.670642 | 15.0 |
| 92 | 02/01/2019 | 11:38:58 Asubuhi | 1.3 | Nala/Dodoma | -6.067298 | 35.662724 | 15.0 |
| 93 | 02/01/2019 | 09:23:15 Usiku | 1.5 | Nala/Dodoma | -6.067511 | 35.668715 | 15.0 |
| 94 | 02/01/2019 | 11:20:08 Asubuhi | 1.9 | Nala/Dodoma | -6.068611 | 35.665504 | 15.0 |
| 95 | 02/01/2019 | 01:54:10 Usiku | 2.0 | Nala/Dodoma | -6.070620 | 35.658200 | 15.0 |
| 96 | 02/01/2019 | 08:00:06 Mchana | 2.1 | Nala/Dodoma | -6.070753 | 35.663971 | 15.0 |
| 97 | 02/01/2019 | 05:02:22 Usiku | 3.5 | Nala/Dodoma | -6.070804 | 35.657998 | 15.0 |
| 98 | 02/01/2019 | 05:52:01 Usiku | 2.0 | Nala/Dodoma | -6.071154 | 35.668206 | 15.0 |
| 99 | 02/01/2019 | 07:31:58 Mchana | 1.5 | Nala/Dodoma | -6.071425 | 35.661656 | 15.0 |
| 100 | 02/01/2019 | 02:21:10 Usiku | 3.4 | Nala/Dodoma | -6.071504 | 35.658556 | 15.0 |
| 101 | 02/01/2019 | 03:48:49 Usiku | 2.8 | Nala/Dodoma | -6.072098 | 35.657718 | 15.0 |
| 102 | 02/01/2019 | 10:52:4 Asubuhi | 2.3 | Nala/Dodoma | -6.072390 | 35.658920 | 15.0 |
| 103 | 02/01/2019 | 08:18:47 Mchana | 2.2 | Nala/Dodoma | -6.072862 | 35.661197 | 15.0 |
| 104 | 02/01/2019 | 06:23:27 Mchana | 1.6 | Nala/Dodoma | -6.072889 | 35.661207 | 15.0 |
| 105 | 02/1/2019 | 11:21:07 Asubuhi | 2.4 | Nala/Dodoma | -6.075751 | 35.654791 | 15.0 |
| 106 | 02/01/2019 | 09:11:43 Usiku | 1.0 | Nala/Dodoma | -6.076821 | 35.653397 | 15.0 |
| 107 | 02/01/2019 | 10:22:57 Asubuhi | 2.0 | Nala/Dodoma | -6.077033 | 35.649167 | 15.0 |
| 108 | 02/01/2019 | 04:50:50 Asubuhi | 2.6 | Nala/Dodoma | -6.078252 | 35.654617 | 15.0 |
| 109 | 02/01/2019 | 03:51:48 Asubuhi | 1.4 | Nala/Dodoma | -6.083082 | 35.649226 | 15.0 |

| S/N | Tarehe | Muda | Kipimo (Richter Scale) | Sehemu | | | DEPTH (KM) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | Eneo lilipotokea | LATITUDE (S ) | LONGITUDE ( E) | |
| 110 | 02/01/2019 | 06:02:30 Mchana | 1.7 | Nala/Dodoma | -6.090467 | 35.643305 | 15.0 |
| 111 | 02/01/2019 | 06:40:57 Mchana | 3.0 | Nala/Dodoma | -6.103341 | 36.693749 | 15.0 |
| 112 | 02/01/2019 | 10:18:50 Usiku | 1.1 | Nala/Dodoma | -6.103841 | 35.630248 | 15.0 |
| 113 | 03/01/2019 | 09:38:10 Usiku | 0.7 | Nala/Dodoma | -6.045537 | 35.730453 | 15.0 |
| 114 | 03/01/2019 | 09:23:22 Usiku | 1.8 | Nala/Dodoma | -6.070704 | 35.661115 | 15.0 |
| 115 | 07/01/2019 | 10:27:10 Jioni | 2.9 | Nala/Dodoma | -6.064024 | 35.674190 | 15.0 |
| 116 | 07/01/2019 | 04:47:07 Usiku | 3.0 | Nala/Dodoma | -6.068495 | 35.659462 | 15.0 |
| 117 | 08/01/2019 | 08:51:37 Usiku | 1.5 | Nala/Dodoma | -6.058328 | 35.686687 | 15.0 |
| 118 | 08/01/2019 | 11:08:02 Asubuhi | 2.0 | Nala/Dodoma | -6.060203 | 35.680939 | 15.0 |
| 119 | 08/1/2019 | 11:08:54 Asubuhi | 1.5 | Nala/Dodoma | -6.062152 | 35.683090 | 15.0 |
| 120 | 08/1/2019 | 07:24:01 Usiku | 1.4 | Nala/Dodoma | -6.073654 | 35.660233 | 15.0 |
| 121 | 08/01/2019 | 01:20:18 Usiku | 2.9 | Nala/Dodoma | -6.077679 | 35.653824 | 15.0 |
| 122 | 09/01/2019 | 09:31:54 Usiku | 1.5 | Nala/Dodoma | -6.053886 | 35.699602 | 15.0 |
| 123 | 09/01/2019 | 09:40:52 Usiku | 1.4 | Nala/Dodoma | -6.070573 | 35.659770 | 15.0 |
| 124 | 09/01/2019 | 09:52:30 Mchana | 2.0 | Nala/Dodoma | -6.075392 | 35.659358 | 15.0 |
| 125 | 09/01/2019 | 12:05:19 Asubuhi | 1.9 | Nala/Dodoma | -6.076304 | 35.659796 | 15.0 |
| 126 | 07/02/2019 | 05:52:38 Asubuhi | 3.7 | Moshi | -3.3005 | 37.3751 | 10.0 |
| 127 | 12/02/2019 | 12:27:07 Jioni | 2.0 | Nala/Dodoma | -6.066167 | 35.667513 | 15.0 |
| 128 | 13/02/2019 | 11:13:01 Asubuhi | 1.4 | Nala/Dodoma | -6.076905 | 35.656097 | 15.0 |
| 129 | 13/02/2019 | 11:20:44 Asubuhi | 2.1 | Nala/Dodoma | -6.079584 | 35.654464 | 15.0 |
| 130 | 14/02/2019 | 03:34:44 Asubuhi | 1.3 | Nala/Dodoma | -.072555° | 35.664669 | 15.0 |
| 131 | 21/03/2019 | 06:15:40Mchana | 5.5 | Msia/Sumbawanga | -7.8777 | 32.0851 | 22 |


**Chanzo:** *Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini Tanzania (GST), 2019*

**Kielelezo Na.1:** *Makusanyo ya Maduhuli kutokana na aina mbalimbali za madini kuanzia mwezi Julai, 2018 – Machi, 2019*





**Chanzo:** *Tume ya Madini, 2019*

**Kielelezo Na.2:** *Makusanyo ya maduhuli kutokana na aina mbalimbali za madini kuanzia mwezi Julai, 2018 – Machi, 2019*





**Chanzo:** *Tume ya Madini, 2019*

**Kielelezo Na.3:** *Kiasi cha dhahabu kilichozalishwa na kuuzwa nje ya nchi na migodi mikubwa ya dhahabu*





**Chanzo:** *Tume ya Madini, 2019*

**Kielelezo Na.4:** *Mwenendo wa Wastani wa Bei ya Madini ya Dhahabu katika Soko la Dunia kuanzia mwaka 2006 - 2018*





**Chanzo:** *London Bullion Market Association (LBMA)*

**Kielelezo Na.5:** *Mwenendo wa Wastani wa Bei ya madini ya Fedha katika Soko la Dunia kuanzia mwaka 2006 - 2018*




***Chanzo:*** *London Bullion Market Association (LBMA)*

**Kielelezo Na.6:** *Ramani inayoonesha vituo nane (8) vya kudumu vya kupimia mitetemo ya ardhi*




***Chanzo:*** *Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini Tanzania (GST), 2019*



Naibu Waziri wa Madini Mhe. Stanslaus H. Nyongo akitazama shughuli za uchimbaji mdogo wa madini ya dhahabu alipotembelea Mgodi wa Wachimbaji wadogo.


JAMHURI YA M
WIZA
MKUTANO MKU
TAREHE: 22 JANUA
UKUMBI MWL. J.K. NYE
MBIU: MADINI
iteko (Mb)